# MAUDHUI YA UKOMBOZI KATIKA *WIMBO MPYA* NA *MSURURU WA USALITI*

**NA**

**ADELINE NDANU KIMEU**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kingine kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

**Adeline Ndanu Kimeu** Tarehe

………………………… …………………………………

(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Dkt. Amiri Swaleh** Tarehe

………………………… …………………………………

(Msimamizi)

**Dkt. Evans M. Mbuthia** Tarehe

………………………… …………………………………

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mume wangu mpendwa, Bw. Joseph Mutiso pamoja na watoto wangu wapendwa Paul Kyengo, Maureen Kasiva na Kelvin Muuo.

## SHUKRANI

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uwezo wa hali na mali ulioniwezesha kuikamilisha safari hii ndefu ya kutafuta shahada ya uzamili na ambayo haikuwa rahisi. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Amiri Swaleh na Dkt. Evans Mbuthia ambao hawakuchoka kamwe kuipitia kazi yangu na kunipa ushauri uliofaa ili kuukamilisha utafiti huu kwa wakati uliofaa. Sitasahau pia kuwashukuru wahadhiri wote walionifunza na kuyafanikisha masomo yangu ya uzamili wakiwemo Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. John Habwe, Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri na Dkt. Prisca Jerono. Mungu awamiminie baraka tele kwa kazi yao bora.

Aidha, nawashukuru wenzangu tuliokuwa pamoja katika darasa la uzamili. Tulishirikiana na kusaidiana vilivyo katika kuikamilisha safari hii. Kamwe siwezi kumsahau rafiki yangu wa dhati Caroline Musyoki tuliyeshirikiana kwa mengi zaidi wakati wa masomo darasani na hata tukiwa nyumbani. Shukrani nyingi pia zimwendee dada yangu Annastacia Kimeu aliyenipa makazi muda huu wote wa masomo.Nawashukuru wazazi wangu wapendwa Simon Kimeu na Theresia Kimeu kwa kuniwekea msingi imara wa masomo nilipokuwa mdogo.

## IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia swala la Maudhui ya Ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kutathmini changamoto zinazozikumba jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa usaliti*, kuchunguza aina tofauti za ukombozi katika riwaya hizi mbili na pia kuonyesha mikakati ya kujikomboa wanayoitumia wanajamii wa *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Utafii huu uliongozwa na nadharia ya U- Marx. Nadharia hii iliasisiwa na Karl Marx na Friedrich Engels kati ya miaka ya 1818 na 1895. Hii ni nadharia ya kiukombozi inayoeleza namna migogoro ya kitabaka hupelekea tabaka la chini kujikomboa kutokana na mfumo wa kibepari unaoendelezwa na tabaka la juu dhidi ya tabaka hili. Utafiti huu uligundua kwamba riwaya za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* zimefaulu katika kuonyesha chanzo cha vita vya ukombozi katika jamii zote mbili. Riwaya hizi zimebainisha kuwa chanzo cha vita vya ukombozi katika jamii hizi kilikuwa ni changamoto zilizowakumba wanajamii hawa. Changamoto zenyewe ni ukoloni, ukosefu wa elimu, utabaka, mvutano baina ya usasa na ukale, dhuluma dhidi ya wanawake, uharibifu wa mazingira, ufisadi, uongozi mbaya na umaskini. Vilevile, utafiti huu ulibainisha kuwa jamii za *Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti* zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika juhudi zao za ukombozi wa aina tofautitofauti kwa kuwa walibuni mikakati ifaayo ya kujikomboa. Ukombozi waliouendeleza wanajamii hawa ni ukombozi unaolenga maswala anuai yanayomzingira mwanadamu yakiwemo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

# YALIYOMO

UNGAMO ........................................................ ii
TABARUKU ........................................................ iii
SHUKRANI ........................................................ iv
IKISIRI ........................................................ v
YALIYOMO ........................................................ vi
ORODHA YA VIFUPISHO VYA ISTILAHI ........................................................ ix

## SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi ........................................................ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ........................................................ 1
1.3 Madhumuni ya utafiti ........................................................ 2
1.4 Nadharia tete ........................................................ 2
1.5 Sababu za kuchagua mada ........................................................ 3
1.6 Upeo na mipaka ya utafiti ........................................................ 3
1.7 Misingi ya Kinadharia ........................................................ 4
1.7.1 Nadharia ya U-Marx ........................................................ 4
1.7.1.1 Mihimili ya Nadharia ya U-Marx ........................................................ 7
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........................................................ 8
1.9 Njia za utafiti ........................................................ 10

## SURA YA PILI:

## SWALA LA UKOMBOZI KATIKA *WIMBO MPYA*

2.1 Utangulizi ........................................................ 12
2.2 Muhtasari wa *Wimbo Mpya* ........................................................ 12
2.3 Changamoto zinazoikumba jamii ya *Wimbo Mpya* ........................................................ 14
2.3.1 Ukoloni ........................................................ 14
2.3.1.1 Ukoloni Mkongwe ........................................................ 14
2.3.1.1.1 Athari za ukoloni mkongwe ........................................................ 15
2.3.1.1.1.1 Uzalendo ........................................................ 15

2.3.1.1.1.2 Usaliti ........16
2.3.1.2 Ukoloni mamboleo ........17
2.3.2 Ukosefu wa elimu ........17
2.3.3 Dhuluma dhidi ya wanawake ........18
2.3.4 Utabaka ........20
2.3.5 Mvutano baina ya usasa na ukale ........21
2.4 Aina za ukombozi katika *Wimbo Mpya* ........22
2.4.1 Ukombozi wa kisiasa ........22
2.4.1.1 Harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe ........22
2.4.1.2 Ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru ........24
2.4.2 Ukombozi wa kielimu ........26
2.4.2.1 Nafasi ya wanawake katika ukombozi wa kielimu ........26
2.4.3 Ukombozi wa kiuchumi ........29
2.5 Hitimisho ........30

**SURA YA TATU**

**SWALA LA UKOMBOZI KATIKA *MSURURU WA USALITI***

3.1 Utangulizi ........32
3.2 Muhtasari wa *Msururu wa Usaliti* ........32
3.3 Changamoto zinazoikumba jamii ya *Msururu wa Usaliti* ........33
3.3.1 Uharibifu wa mazingira ........33
3.3.2 Ukoloni ........34
3.3.2.1 Swala la ukoloni mkongwe katika *Msururu wa Usaliti* ........34
3.3.2.2 Swala la ukoloni mamboleo katika *Msururu wa Usaliti* ........36
3.3.3 Ufisadi ........38
3.3.4. Umaskini ........40
3.3.5 Uozo wa jamii ........41
3.3.5.1 Mauaji ........41
3.3.5.2 Ubakaji ........43
3.3.5.3 Uasherati na uzinzi ........43
3.3.6 Utabaka ........45
3.3.7 Uongozi mbaya ........46

3.4. Ukombozi katika *Msururu wa Usaliti* ........................................................ 47
3.4.1 Aina za ukombozi katika *Msururu wa Usaliti* ........................................48
3.4.1.1 Ukombozi wa kimazingira ........................................................48
3.4.1.1.1 Nafasi ya wanawake katika ukombozi wa kimazingira........................49
3.4.1.2 Ukombozi wa kisiasa ........................................................52
3.4.1.2.1 Harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe............................52
3.4.1.2.2 Ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru ........................................53
3.4.1.2.2.1 Nafasi ya vijana katika ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru ............54
3.4.1.3 Ukombozi dhidi ya ufisadi ........................................................55
3.4.1.3.1 Nafasi ya vijana katika ukombozi dhidi ya ufisadi................................55
3.4.1.4 Ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa ........................................57
3.4.1.4.1 Nafasi ya vijana katika ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa ......59
3.4.1.5 Ukombozi dhidi ya uozo wa jamii ........................................................60
3.4.1.5.1 Ukombozi dhidi ya mauaji ........................................................60
3.4.1.5.2 Ukombozi dhidi ya ubakaji ........................................................61
3.4.1.5.3 Ukombozi dhidi ya uasherati na uzinzi ........................................61
3.5 Hitimisho ........................................................ 62

**SURA YA NNE**

**MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

4.1 Utangulizi ........................................................ 64
4.2 Muhtasari wa matokeo ........................................................ 64
4.3 Hitimisho ........................................................ 70
4.4 Mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye ........................................................ 70
**MAREJELEO** ........................................................ 71

## ORODHA YA VIFUPISHO VYA ISTILAHI

**DDT:** Dichlorodiphenyltrichloroethane

**GBM:** Green Belt Movement

**JEMA:** Jeshi la Mazingira

**NCWK:** National Council of Women of Kenya

**UNICEF:** United Nations Children's Education Fund

**UWATA:** Umoja wa Wazalendo wa Taifa

**WHO:** World Health Organization

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza Maudhui ya Ukombozi katika riwaya mbili za Mwenda Mbatiah ambazo ni *Wimbo Mpya* (2004) na *Msururu wa Usaliti* (2010). Ukombozi katika nchi nyingi za bara la Afrika ulianza tangu wakati wa Vita vya pili vya Ulimwengu. Waafrika wengi walikuwa wameshiriki vita hivi kwa niaba ya mataifa ya kikoloni. Tajriba waliyoipata katika kipindi hiki ilianzisha mwamko mpya baada ya wao kusalitiwa na wakoloni. Wakaanza kuona kwamba pia wao wangeweza kupigania maslahi yao. Katika miaka ya sitini, mabadiliko yalianza kutokea barani Afrika. Ilikuwa miaka ya harakati za ukombozi na uhuru kwa nchi nyingi za bara hili.

Wabeba kurunzi wa awamu hii ya kwanza ya ukombozi walikuwa viongozi Waafrika waliokuwa na maono juu ya Afrika tarajiwa kwa kizazi chao na vizazi vijavyo. Kilikuwa kipindi cha matumaini makubwa na kujiamini kwamba, uhuru na umoja vingetatua matatizo yote ya umaskini, ujinga na maradhi.Viongozi waliochukua hatamu za uongozi waliwasaliti wananchi waliowapatia mamlaka ya kuwaongoza. Kwa hivyo, katika nchi nyingi za Afrika, uhuru ukakosa maana iliyotarajiwa na kuwa kama uhuru wa bendera tu.

Katika riwaya hizi mbili, maudhui ya ukombozi yaliyojitokeza ni ukombozi wa kimazingira, ukombozi wa kisiasa, ukombozi wa kielimu, ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa, ukombozi dhidi ya uozo wa jamii, ukombozi dhidi ya ufisadi na ukombozi wa kiuchumi.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Watafiti wengi wamelishughulikia swala la ukombozi. Baadhi ya watafiti hawa wamelishughulikia swala hili kama mojawapo ya maudhui katika kazi mbalimbali za kifasihi huku wengine wakionyesha jinsi ukombozi ulivyotokea katika matukio ya kihistoria. Licha ya kuwa na tafiti kuhusu swala la ukombozi katika kazi mbalimbali za kifasihi, swala hili bado ni muhimu katika maisha ya binadamu ambaye kila uchao huwa katika harakati za kujinasua dhidi ya changamoto zinazomkabili. Hata baada ya binadamu kujikomboa kutokana na changamoto fulani, yeye huzidi kukumbwa na changamoto mpya ambazo humlazimu kujikomboa dhidi yake ili kuwa huru.

Jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* zilikumbwa na changamoto ya ukoloni mkongwe. Ni kutokana na hali hii ambapo jamii hizi zilijiingiza katika harakati za kujikomboa ili ziweze kupata uhuru. Baada ya uhuru, viongozi waliochukua hatamu za uongozi waliwasaliti wanajamii hawa kupitia kwa uongozi mbaya. Waliyajali maslahi yao wenyewe huku wananchi wao wakizidi kuteseka. Kwa hivyo, uhuru katika jamii hizi ulipoteza maana na kugeuka kuwa uhuru wa bendera tu. Vilevile, wanajamii hawa walizidi kukumbwa na changamoto zaidi huku ukoloni mamboleo ukisheheni na kuwa sehemu ya mfumo wa uongozi katika jamii hizi.

Kutokana na haya, utafiti huu ulilenga kuonyesha juhudi za wanajamii wa *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* za kujikomboa kutokana na changamoto nyingi zilizowakabili katika vipindi vya kabla na baada ya uhuru. Juhudi hizi ziliongozwa na vijana wasomi ili kujaribu kuunda jamii mpya zilizokuwa na uhuru kamili na wa kweli hasa baada ya kupata uhuru wa bendera kutoka kwa wakoloni.

## 1.3 Madhumuni ya utafiti

Tunadhamiria kuchambua na kuchanganua riwaya za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* kwa kuangazia maudhui ya ukombozi ili:

i. Kutathmini changamoto zinazozikumba jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*.
ii. Kuchunguza aina tofauti za ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*.
iii. Kuonyesha mikakati ya kujikomboa inayotumiwa na wanajamii wa *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*.

## 1.4 Nadharia tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Kazi za Mbatiah za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* zimefaulu katika kuonyesha chanzo cha vita vya ukombozi katika jamii hizi mbili.
ii. Jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* zitafanikiwa katika harakati zao za ukombozi wa aina tofautitofauti.
iii. Mikakati ya kujikomboa wanayoitumia wanajamii wa *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* itafanikisha ukombozi.

### 1.5 Sababu za kuchagua mada

Tulivutiwa na somo hili kuhusu ukombozi kwa sababu limebakia kuwa swala muhimu katika jamii nyingi. Mataifa ya Ulimwengu wa Tatu yalipitia hali ngumu chini ya ukoloni mkongwe. Kwa hivyo, juhudi zao za kupigania ukombozi zilikusudiwa kujiondolea matatizo haya. Katika mataifa hayo, mashujaa waliochukua hatamu za uongozi walitegemewa kuangamiza matatizo haya, lakini katika mataifa mengine, matatizo haya hayakuchukuliwa kwa uzito na hata uongozi wa baada ya uhuru ukashindwa kutatua baadhi ya matatizo ya raia na kuwafanya kuanzisha juhudi za ukombozi mara nyingine.

Baada ya wakoloni kuingia katika jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*, wanajamii hawa waliteseka sana chini ya uongozi wa wakoloni. Mambo haya yalidhihirika kupitia kupokonywa ardhi yao iliyokuwa na rotuba, kufanyishwa kazi ngumu kwenye mashamba ya wazungu, kulipa kodi ambayo hawangeweza kuimudu, kubebeshwa kipande na maovu mengineyo. Ni kutokana na hali hii ambapo jamii hizi zilihitaji kujikomboa na kuongozwa na viongozi Waafrika wenzao.

Aidha, baada ya uhuru, wanajamii hawa waliamini kuwa wangeweza kujitawala na kujiendeleza tena. Hali hii haikutimia kwa sababu Waafrika waliochukua hatamu ya uongozi hawakutimiza matakwa ya wanajamii. Kwa hivyo, uhuru katika jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* haukuleta mabadiliko yaliyokusudiwa. Uhuru huu ulibakia kuwa wa bendera tu, huku ukoloni mamboleo ukichukua nafasi kubwa katika uongozi wa mataifa hayo. Licha ya jamii hizi kupeperusha bendera, wananchi wao walizidi kufungwa pingu za umaskini, ujinga na magonjwa. Kutokana na haya, jamii hizi zilihitaji ukombozi dhidi ya shida zilizowakabili baada ya uhuru na pia kuuondoa ukoloni mambo leo ili uhuru kamili upatikane.

### 1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa maudhui ya ukombozi katika riwaya za *Wimbo Mpya* (2004) na *Msururu wa Usaliti* (2010). Aidha, kazi nyingine zilipitiwa ili kuutia nguvu uchanganuzi wetu lakini hazikuwa sehemu ya kimsingi ya kazi hii. Mifano hii ilitumika pale tu ilipobidi ili kuhimili uchanganuzi wa riwaya teule.

## 1.7 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu ni wa kifasihi na hivyo basi tuliongozwa na nadharia ya kifasihi. Kimsingi, utafiti wetu ulitumia nadharia ya U-Marx. Nadharia hii ilitumika kuchanganua maudhui ya ukombozi katika riwaya mbili tulizoziteua.

### 1.7.1 Nadharia ya U-Marx

Nadharia ya U-Marx iliasisiwa na Karl Marx ( 1818-1863) na Friedrich Engels (1820-1895). U-Marx ni dhana inayolenga maswala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, na kitamaduni. Inajadili uhusiano na mapambano ya kitabaka kati ya watu wa tabaka la chini dhidi ya wale wa tabaka la juu. Pia hujishughulisha na kumulika njia kuu za uzalishaji mali na maendeleo ya kijamii katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu. Mfumo wa uzalishaji mali katika hali halisi ya maisha ndio unaozielekeza hali za kijamii, kisiasa, kichumi na kitamaduni. Mabadiliko ya kiuchumi yatokeapo, muundo mzima wa taasisi ya kijamii hubadilika.

Kulingana na mtazamo wa U-Marx, jamii za ulimwengu zimepitia hatua mbalimbali za kihistoria katika nyakati tofauti. Hatua hizi zinahusiana na njia za uzalishaji mali. Hatua ya kwanza ilikuwa ni mfumo wa ishitiraki ambapo binadamu aliishi kwa ushirika huku kila mtu akifanya kazi ambayo ingeifaidi jamii. Jamii zilipoendelea, zilianza biashara ndogondogo na mataifa jirani. Mara uzalishaji mali ukalenga katika mahitaji ya jamii na biashara. Wakati huu, mali ilitengwa na wale walioshiriki katika kuizalisha. Baada ya muda, mfumo wa uzalishaji mali ulibadilika na kuwa wa kibwanyenye. Mfumo huu ulijitambulisha kwa ubadhirifu na ufujaji miongoni mwa tabaka tawala.

Maisha ya tabaka hili yalikuwa ni ya matumizi tu bila kushiriki katika uzalishaji mali. Jambo hili lilizua maendeleo ya tabaka la kibepari lililokuwa la kimapinduzi kwa sababu lilileta mfumo mpya wa kiuchumi uliojulikana kama mfumo wa kibepari. Hali hii imeleta mikinzano mikali sana ya kitabaka. Wataalamu wengine pia wametoa mchango wao kuhusiana na U-Marx.

Kwa mujibu wa Lunacharsky (1973) “U-Marx una jukumu kubwa, tena la msingi, kujishughulisha kwa dhati na juhudi katika namna ya kumuumba mtu mpya na mfumo mpya wa maisha” (uk. 10).

U-Marx unayachukua maisha ya kijamii kuwa muunganiko kamili, ambao viungo mbalimbali hutegemeana na kukamilishana, inavyoelekea upya wa mtu na mfumo anaoujadili.
Kulingana na Williams (1977), nadharia hii inamhitaji msanii na mhakiki kujadili suala la itikadi tawala, utamaduni, mihimili ya dola na ya kiuchumi kwa namna ambayo itawafungua fikra, hisia na macho wanaonyimwa na kunyanyanyaswa, ili kutambua kuwa vitu hivi ndivyo vyanzo vya ukandamizaji na unyonyaji.

Wamitila (2006) ameelezea U-Marx kama falsafa ya kiuyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali za kiuyakinifu za maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. Hii ina maana kwamba Marx hayategemezi mawazo yake kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto, bali anayategemeza kwenye uhalisia unaoonekana.

Uhakiki wa Ki-Marx unatambulishwa na mtazamo wa uhalisia unaoonyesha mkubaliano fulani na kuegemezwa kwenye mawazo ya mwanafalsafa wa Kijerumani Karl Marx. U-Marx unahusu nyanja mbalimbali za maisha kama vile uchumi, historia, jamii na mapinduzi. Msukumo mkubwa wa nadharia hii umewekewa misingi na kauli aliyoitamka Marx, akimzungumzia mwanafalsafa Februch kuwa "wanafalsafa wameishia kuufasiri ulimwengu tu, lakini jambo muhimu ni kuubadilisha."

U-Marx umeendelezwa hadi  miaka ya hivi karibuni. Terry Eagleton (2011) ni mmoja wa wale wanaoiendeleza nadharia hii. Katika kitabu chake, "*Why Marx was Right*,"anaonelea kuwa unyonyaji wa kibepari ni mfumo wa ulafi, ukandamizaji na uangamizaji na anaushtumu vikali.

Kulingana na Eagleton, ubepari kama mfumo wa mashindano ya kiuchumi na ambao ni wa kuangamiza ndio unaosababisha kiwango cha juu cha kutoajiriwa na matokeo yake huwa ni uhalifu mwingi unaowafanya wahalifu kufungwa katika magereza ya Kimagharibi.  Kwa kudumisha viwango vya chini vya ujira, waajiri wa kibepari hutofautiana na wafanyikazi wa kiwango cha chini wanaojaribu kupigania haki zao ili ujira wao uongezewe, hivyo basi, kusababisha mapinduzi ya Ki-Marx. Matokeo ya mfumo wa mapambano ya kitabaka anaoufuata Eagleton ni kuwa wafanyikazi wa kiwango cha chini wana hamu ya kupata mgao sawa wa faida

na ambao husababisha watu wengi kutoajiriwa kwa kuwa wafanyikazi wa kiwango cha chini hupendekeza serikali iwe na sheria kuhusu kiwango cha chini zaidi cha ujira. Kutokana na haya, tabaka jipya lisiloonekana na manabii wa Ki-Marx na ambalo ni tabaka la watu wengi wasioajiriwa huzuka.

Tabaka la wafanyikazi linalonyonywa kila wakati huamini kuwa litafaidika kutokana na juhudi zao za kusukumia juu ada zao za ujira hata ikiwa uzalishaji wa bidhaa ni wa kiwango cha chini. Eagleton anaelezea ndoto yake isiyokamilika kuhusu jamii yenye matabaka ya kategoria nne. Kategoria ya kwanza ni ya watawala ambao humiliki njia za uzalishaji mali. Kategoria ya pili ni ya mabwanyenye wa kiwango cha kati huku kategoria ya tatu ikiwa ya kiwango cha chini kati ambacho ni cha mabwanyenye uchwara. Kategoria ya nne ni ya wafanyikazi.

Eagleton anakosa kuona kuwa wafanyikazi wa ujira wanaonyonywa ndio wanaopinga kuajiriwa kama wafanyikazi wa kudumu kwa kusingizia imani za kibepari kuwa "ulafi ni mzuri." Kwa kusukumia juu ujira na kuunda miungano imara ya wafanyikazi, haki chache za wafanyikazi wa kiwango cha chini waliojiriwa huwafanya wapuuze matakwa ya kibinafsi ya wale wasioajiriwa kwa kugawanya faida zinazotokana na viwanda kati ya wafanyikazi wachache. Kwa kifupi, Eagleton anapendekeza mfumo wa kiuchumi ambao unaweza kuthibitiwa na watu wote katika jamii. Anatuhakikishia kuwa elimu na usimamizi mzuri wa nchi unaweza kupunguza athari za ubepari.

Kwa upande mwingine, Eagleton anaonelea kuwa matatizo ya kiuchumi yaliyopo katika jamii nyingi yanatokana na ubepari kama mfumo wa uzalishaji mali. Kulingana na Eagleton, U-Marx hautoi ahadi zozote juu ya binadamu asiye na kasoro, bali unashikilia kuwa mashindano katika maisha ya binadamu yataendelea. Kwa maoni yetu, Eagleton amechukua jukumu la kuuendeleza U-Marx ulioasisiwa na Karl Marx na Friedrich Engels. Hii ni kwa kuwa mawazo yake katika kazi yake hayatofautiani na yale ya Marx, bali anayatilia nguvu mawazo yenyewe.

Kwa jumla, wataalamu wote tuliowataja hapa na ambao wameizungumzia nadharia ya U-Marx wanasisitiza sana kuhusu ukombozi wa tabaka la chini dhidi ya tabaka la juu ambalo ndilo

huchukua nafasi kubwa katika kuitawala na kuiongoza jamii. Ukombozi huu unaweza kuafikiwa iwapo wanajamii wa tabaka la chini wataungana na kushirikiana katika juhudi zao za kuuangamiza mfumo wa utawala wa tabaka la juu. Vilivile, tabaka hili linafaa kubuni mikakati ifaayo ya kukabiliana na tabaka la juu ili kuuvunjilia mbali mfumo wao wa ubepari.

#### 1.7.1.1 Mihimili ya Nadharia ya U-Marx

Kwa mujibu wa Wamitila (2006), nadharia ya U-Marx inaongozwa na mihimili ifuatayo:

i. Historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo itachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi na pia huathiri uzalishaji mali na usambazaji wa mali hizo. Hivi vyote hunda msingi ambapo kwenye msingi huo ndiko kunakotengemezwa muundo wa juu au “kikorombwezo.” Kikoromwbezo ndicho kinachohusisha maadili, itikadi, dini, utamaduni na mengineyo.

ii. Wahakiki wa Ki-Marx wanaamini kwamba daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi-jamii. Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni harakati za kitabaka. Hatua ya juu ya mwendeleo wa utabaka ni uzukaji wa mfumo wa ubepari ambapo mali humilikiwa na watu wachache. Mali hii inapatikana kutokana na unyonyaji wa umma; hasa wafanyikazi.

iii. Matamanio na matakwa ya matabaka yaliyopo katika jamii na hasa tabaka lenye nguvu yanaakisiwa katika itikadi iliyopo katika jamii, jinsi na miundo ya mawazo ambayo aghalabu huwa imeshika kwa nguvu na huwapo kila mahali kiasi cha kuwa huenda wanajamii wasiitambue kwa haraka.

iv. Ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali kutokana na juhudi za wafanyikazi au wenyewe utaishia kujiangamiza kutokana na mbegu za maangamizi unazozisheheni.

v. Njia ya kusaidia na labda kuharakisha kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushtumu, kulaumu na kufichua batili iliyopo katika itikadi za kibwanyenye inayouimarisha ubepari. Hili huwa jukumu muhimu la waandishi wa kifasihi ambapo kazi zenye mwelekeo huu hufichua ubaya na uovu wa mvumo huo.

vi. Nadharia ya Ki-Marx inapaswa kuhusishwa na kuandamana pamoja na hata kuelekeza kwa matendo ya kiutekelezaji dhidi ya mfumo mzima wa kiubepari.

Kwa jumla, nadharia ya U-Marx inajihusisha na mapambano kati ya matabaka mawili ambayo ni tabaka la wanyanyaswao na lile la wanyanyasaji ili tabaka la wanyanyaswao liweze kujikomboa na kujenga jamii mpya ambayo inaweza kujisimamia na kujiendeleza. Katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*, matabaka haya mawili yanadhihirika na ndio chanzo cha harakati za ukombozi.

Katika utafiti wetu, mihimili hii yote ni muhimu kwa kuwa inaafikiana na utafiti wetu.

**1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Watafiti waliotutangulia wametoa michango yao tofautitofauti kuhusu masuala ya ukombozi. Mugambi (1983) amehakiki Kilio cha wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed zifuatazo: *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980) *na Dunia Mti Mkavu* (1980). Katika kazi hii, anatuonyesha jinsi wanyonge wanavyodhalilishwa katika jamii. Kazi hii inahusiana na yetu kwa kuwa ilitupatia uelewa mzuri wa dhuluma zinazotendwa na viongozi dhidi ya wananchi wa kawaida katika jamii husika. Dhuluma hizi ndizo zinazojadiliwa katika jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti,* na ndizo ambazo zinapelekea kuanza kwa juhudi za ukombozi wa jamii hizi. Hivyo basi, kazi hii ilitupa mwelekeo mzuri katika uchanganuzi wetu.

Mazrui (1984) *amehakiki Dunia Mti Mkavu* kwa kutumia nadharia ya U- Marx. Ameichanganua riwaya hii kwa misingi ya kisiasa na kijamii kuhusu mabadiliko ya upembuzi wa jamii za Kiafrika chini ya utawala wa kiistimari. Uhakiki huu ulitupa uelewa hasa kuhusu misingi ya kuwepo kwa ukombozi, suala ambalo lilitufaa katika uhakiki wetu.

Njogu (1987) ameshughulikia maudhui ya mapinduzi katika riwaya za visiwani Zanzibar kwa kutumia nadharia ya U-Marx. Hizi ni riwaya za Mohamed Suleiman Mohamed, Said Ahmed Mohamed na Shafi Adam Shafi. Riwaya zenyewe ni *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978*), Kuli* (1979), *Asali Chungu* (1978), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980), *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976). Katika kazi yake, amezichanganua hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii zilizoyaleta mapinduzi ya 1964. Kulingana na Njogu, mtazamo wa fasihi Ki- Marx unaonyesha uhusiano wa fasihi na uzalishaji mali. Mapinduzi ya kijamii yatokeapo na kufaulu, mfumo wa uzalishaji mali aghalabu hubadilika na taasisi za kitamaduni, fasihi ikiwepo huchukua mkondo mwingine. Kadri mfumo wa uzalishaji mali unavyobadilika ndivyo fasihi nayo idhihirishavyo

mabadiliko hayo katika tanzu zake zote. Mabadiliko haya yote yanaonyeshwa vyema na mtazamo wa Ki-Marx. Hivyo basi, kazi hii ilituelekeza katika kuyachanganua maudhui ya ukombozi wa kisiasa katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti.*

Karanja (1990) amezihakiki tamthilia za kiukombozi *za Mzalendo Kimathi*, *Mukwava wa Uhehe* na *Kinjeketile*. Amezihakiki tamthilia hizi ili kubaini taswira yakinifu ya Mwafrika katika vita vya ukombozi. Uhakiki wake unaonyesha kuwa fasihi haina budi kuwa yakinifu ili itimize lengo lake la ukombozi. Aidha, anatuonyesha kuwa tamthilia tatu alizozichagua katika tasnifu hii zimemchora Mwafrika kiuyakinifu katika vita vya ukombozi. Mawazo haya yalitufaa katika kuishughulikia mada yetu ya maudhui ya ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* ambazo ni riwaya zinazomlenga Mwafrika katika swala la ukombozi.

Kiongera (2012) ameshughulikia mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia za Kiswahili zifuatazo: *Kifo Kisimani* na *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* za Kithaka wa Mberia na *Pango* na *Seserumbe* za Wamitila akitumia nadharia ya Ki- Foucault, iliyoasisiwa na Micheal Foucault. Katika sura ya pili, anachunguza maovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yanayoendelea katika jamii husika. Anawaonyesha vijana wakikabiliana na maovu hayo ili kuleta mabadiliko chanya. Aidha, katika sura ya tatu anachunguza mafanikio waliyopata vijana katika kubadilisha jamii zao. Hata ingawa utafiti huu umejikita katika tamthilia, utafiti wetu umejikita katika riwaya. Utafiti huu ulitufaa sana katika uchanganuzi wetu wa maudhui ya ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Kazi hizi zinahusiana pakubwa kwa kuwa zinaonyesha nafasi ya vijana katika ukombozi wa jamii, ingawa hatuchunguzi nafasi ya vijana pekee katika ukombozi bali uhusika wa jamii nzima.

Kipyegon (2013) katika tasnifu yake, “Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke katika *Natala* na *Kifo Kisimani*,” amemsawiri mwanamke akinyanyaswa katika jamii ya ki- ubabedume. Ametumia nadharia ya Ufeministi katika uchanganuzi wake. Anaonyesha vile mwanamke anavyochukiwa katika jamii. Licha ya hayo, juhudi za mwanamke za kujikomboa na kupata hadhi katika jamii zimeangaziwa. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa kuwa katika jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*, wanawake wanachukua nafasi kubwa katika harakati za

kuzikomboa jamii hizi. Utafiti huu pia ulituelekeza katika kuyachanganua maudhui ya ukombozi wa kimazingira na wa kielimu.

Sabula (2014) ameshughulikia swala la " Nafasi ya Wanawake Katika Uhifadhi wa Mazingira Katika riwaya ya *Nakuruto*." Utafiti huu umetumia mtazamo wa fasihi ya Ufeministi wa Kiekolojia. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kupambanua mchango wa ufeministi wa Kiekolojia katika uhifadhi wa mazingira katika riwaya ya *Nakuruto*, kumpambanua mhusika Nakuruto na mchango anaoutoa katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, kujadili kwa kina changamoto anazozipitia mwanamke katika kuhifadhi mazingira, kujadili athari za masuala ya kimazingira na jinsi zinavyojitokeza katika riwaya hii. Utafiti huu ulibainisha kwamba, Ufeministi wa kiekolojia una nafasi ya kuwazindua wanawake ili kuleta ukombozi wa kimazingira. Utafiti huu ulichangia pakubwa katika kuchanganua maudhui ya ukombozi wa kimazingira katika riwaya ya *Msururu wa Usaliti* kwa kuwa mhusika anayeongoza jamii katika ukombozi wa kimazingira ni mwanamke.

Osangu (2015) ameshughulikia ukombozi wa kisiasa na kiuchumi katika *Mkamandume* kwa kutumia nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. Maudhumuni ya utafiti huu yalikuwa kutathmini maswala yaliyopelekea mapinduzi ya mwaka wa 1964 na athari zake kwa watu wa Zanzibar na Pemba kulingana na *Mkamandume.* Utafiti huu uligundua kwamba, matatizo yanayowakumba wananchi wa visiwani Zanzibar na Pemba yana misingi yake katika historia ya jamii hii. Kulingana na *Mkamandume*, hali ya kisiasa na kichumi iliendelea kuwa mbaya zaidi baada ya mkoloni kuondoka kiasi cha kuwepo kwa haja ya ukombozi wa pili. Utafiti huu ulitufaa sana katika uchanganuzi wa swala la ukombozi wa kisiasa katika riwaya zetu teule.

**1.9 Njia za utafiti**

Utafiti wetu ulikuwa wa maktabani. Tulizisoma riwaya za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* kwa makini na kuchanganua maudhui yote ya ukombozi yaliyojitokeza katika riwaya hizi. Aidha, tulisoma makala, vitabu na maandishi yanayohusu nadharia ya U-Marx kwa kuwa ndiyo nadharia tuliyoitumia katika utafiti wetu. Tulifanya juhudi za kuielewa nadharia hii na mihimili yake mikuu na kuelewa namna ya kuitumia katika kuhakiki riwaya tulizoziteua. Tulirejelea makala na tasnifu mbalimbali zilizoandikwa kuhusu ukombozi katika kazi za kifasihi. Pia

tulijikita katika tovuti kwenye mitandao tofauti ili tupate marejeleo zaidi kuhusu nadharia ya U-Marx. Mwisho, tulishirikisha maoni ya wataalamu katika taaluma hii kuhusiana na mada yetu ya utafiti pamoja na kuufuata ushauri kutoka kwa wasimamizi wetu na wahadhiri wengine.

## SURA YA PILI

## SWALA LA UKOMBOZI KATIKA *WIMBO MPYA*

### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia swala la ukombozi katika *Wimbo Mpya*. Katika kufanya hivi, kwanza tumetoa muhtasari wa riwaya hii ili kufafanua taswira kamili ya jamii yenyewe.Vilevile, tumezishughulikia changamoto zinazoikumba jamii hii ndipo ianze kujishughulisha katika harakati za ukombozi. Changamoto ambazo tumezishughulikia ni ukoloni, ukosefu wa elimu, dhuluma dhidi ya wanawake, utabaka na kisha mvutano baina ya usasa na ukale. Hatimaye, tumeshughulikia aina za ukombozi katika *Wimbo Mpya* ambazo ni ukombozi wa kisiasa, ukombozi wa kielimu na ukombozi wa kiuchumi.

### 2.2 Muhtasari wa *Wimbo Mpya*

*Wimbo Mpya* ni riwaya inayoangazia juhudi za ukombozi dhidi ya ukoloni zikiongozwa na mhusika mkuu Meja Marete ambaye alikuwa kiongozi wa kundi la kupigania uhuru alililoiita "Jeshi la Wazalendo." Mwanzoni, kikosi cha Meja Marete kilionekana kufaulu katika pambano kubwa na la mwisho ambalo lilitokea katika kipindi cha tangu mwaka wa 1952, hali ya hatari ilipotangazwa, hadi 1956, ambapo vita vya uhuru vilipamba moto. Hili lilikuwa pambano gumu na kali ambalo waliliita "Gharika la damu."

Kufaulu kwa kikosi hiki katika vita vya upiganiaji uhuru mwanzoni kuliletwa na matumizi ya bunduki bora na ambazo zilikuwa miongoni mwa zile walizowanyang'anya askari wa Kikoloni baada ya kuwaua. Aidha, wapiganaji wengine walikuwa na bunduki zilizotengenezewa msituni na wapiganaji wenyewe. Hatimaye, jeshi la wakoloni lililipiza kisasi na kusababisha vifo vya baadhi ya wapiganaji wa jeshi la wazalendo. Jambo hili lilisababisha kutawanyika kwa jeshi la wazalendo na hatimaye walirudi kambini mwao. Shughuli ya kupigania uhuru haikuwa rahisi kwani iliwabidi wapiganaji kuishi msituni muda wote wa upiganiaji uhuru ili kujihakikishia usalama wao. Hii ilitokana na hali kuwa wapiganaji hawa waliwindwa usiku na mchana na jeshi la wakoloni ili waweze kushikwa ndio wakomeshe vita vya upiganiaji uhuru. Hali hii ndiyo aliyokumbana nayo Meja Marete na ambayo haikuwa ya kuvutia kwake. Ilimbidi aende nyumbani kwake usiku huku akiwa amejificha ili kupata chakula na nguo za kubadilisha na

kurudi msituni wakati huo huo. La mno ni kwamba hata alipofika kwake, aliongea kwa mnong'ono ili asiweze kutambulikana kwani alikuwa mmoja wa wale waliowindwa zaidi na askari wa Kikoloni. Jambo hili lilimtia wasiwasi mwingi Nkirote aliyekuwa mkewe Meja Marete kwa sababu hakuweza kubainisha ni lini mumewe angerudi nyumbani na kuishi nao kama familia. Naye Meja Marete kwa upande wake hakupendelea kurudi nyumbani kabla ya uhuru kupatikana kwani alionelea kuwa akifanya hivyo atakuwa ameipoteza miaka yote aliyokuwa mwituni na atakuwa ameisaliti harakati nzima ya upiganiaji uhuru.

Vita viliendelea hadi mwaka wa 1963 ambapo uhuru ulipatikana na taifa jipya kuzaliwa. Cha kushangaza ni kuwa baada ya uhuru, baadhi ya wapiganiaji uhuru akiwepo Meja Marete walidai kuwa hawakupata walichokuwa wakipigania na hivyo waliamua kuendelea kuishi msituni hadi wakati haki ingetendeka. Walidai kuwa ardhi yao iliyokuwa imechukuliwa na masetla ilifaa kurudishwa ili haki itendeke; jambo ambalo halikutekelezwa. Meja Marete alikaa mwituni hadi pale ambapo mkewe aliyekuwa mgonjwa alizidiwa na ugonjwa wake kiasi cha kulazwa hospitalini.

Kutokana na hali hii, Mwathi ambaye alikuwa mzee wa kijiji aliwaita wanakijiji kadhaa ili kushughulikia jambo hili la dharura. Wanakijiji hawa waliamua kuwa msafara wa kwenda kumtafuta Meja Marete ili kumrudisha nyumbani ndipo aweze kumshughulikia mkewe ungeongozwa na Igweta, Rogere, Getimbo na Bi. Mariamu ambaye alikuwa mwanamke shujaa. Ingawa safari ilikuwa ngumu, hatimaye walimpata Meja Marete na akakubali kurudi na wao. Walipofika nyumbani, walipata kuwa bibi yake aliaga siku iliyotangulia. Wanakijiji hawa walijishughulisha na harakati za mazishi na hatimaye wakamzika bibiye Meja Marete.

Baada ya uhuru, Bi Mariamu aliongoza juhudi mpya za kuiendeleza jamii kupitia uzinduzi wa mradi wa kujenga shule ya msingi kijijini mwao. Kupitia kwa juhudi za Bi. Mariamu akisaidiana na wanakijiji, mradi wa shule ulianza na kijiji chote kikashirikiana katika kutoa vifaa vya ujenzi na ujenzi wenyewe. Hatimaye, shule ilimalizika na wanafunzi wakaanza kusomea katika shule hii. Bi Mariamu aliyekuwa mwalimu naye alipata uhamisho na kuja kuanza kufunza katika shule hii aliyoianzisha mwenyewe.

Ujenzi wa shule hii ulipiga hatua kubwa kimaendeleo kwani kila ijumaa, akina mama wa kijiji cha Gaito na vijiji vingine walikutania katika shule hii ili kupanga miradi ya kujiendeleza wakiongozwa na Bi. Mariamu kama mwenyekiti wao. Maendeleo haya yalimpa Bi. Mariamu sifa kuanzia vijijini hadi mijini na hata bungeni.

### 2.3 Changamoto zinazoikumba jamii ya *Wimbo Mpya*

Wakoloni walipoingia barani Afrika, Waafrika walikumbana na changamoto nyingi chini ya utawala mpya wa serikali za kikoloni. Baada ya uhuru, kulikuwa na matumaini makubwa kuwa mambo yangebadilika kutokana na wananchi kuongozwa na viongozi Waafrika wenzao. Punde tu baada ya uhuru, mambo yalianza kwenda kinyume na changamoto mpya zikaanza kuzuka.

Jamii ya *Wimbo Mpya* vilevile ilikumbwa na changamoto mbalimbali kabla na hata baada ya uhuru. Baadhi ya changamoto hizi ni ukoloni, ukosefu wa elimu, dhuluma dhidi ya wanawake, mvutano baina ya usasa na ukale na utabaka.

#### 2.3.1 Ukoloni

Ukoloni ni mfumo wa taifa moja kutawala maeneo mbalimbali yanayokaliwa na watu wengine katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na hata kijamii. Aidha, ni mfumo wa jamii moja kuitawala jamii nyingine na kufilisi rasilimali za nchi hiyo tawaliwa. Ukoloni katika riwaya hii umegawika katika awamu mbili ambazo ni ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo.

##### 2.3.1.1 Ukoloni Mkongwe

Ukoloni mkongwe ni hali ambapo mataifa yenye uwezo mkubwa kama vile Marekani, Ufaransa, Uhispania na mengineyo yaliyavamia mataifa mengine ambayo hayakuwa na uwezo; hasa mataifa ya bara Afrika na kuyatawala kwa nguvu za kijeshi kupitia kwa njia ya kupigana vita na mataifa hayo. Madhara mengi yalisababishwa na ukoloni mkongwe barani Afrika yakiwemo Waafrika kunyanyaswa na hata kuuawa kwa wingi na wakoloni. Wabeberu hawa pia waliupora utajiri wa Afrika na kuwageuza Waafrika kuwa vibarua katika mashamba ya Wazungu. Aidha, Waafrika walitendewa vitendo vya dhuluma na ukatili na hata viwanda na teknolojia waliyokuwa nayo wakati huo kuvurugwa na wakoloni hao. Kwa njia hii, yaliyokuwa mema ya Afrika yalipotea, yakadharauliwa na hata kubezwa na wabeberu.

Hata hivyo, sio kila kitu walichokifanya wakoloni kilikuwa kibaya kwa Waafrika. Kulikuwa na mambo mengine mazuri ya kuigwa. Kwa mfano, wakoloni waliwafunza Waafrika jinsi ya kupanda mimea mipya ambayo hawakuwa wakiipanda hapo awali. Aidha, mashule yalianzishwa na baadhi ya Waafrika kunufaika kutokana na kupata elimu katika mashule hayo. Wakoloni pia walijenga mahospitali ambayo waliyaacha kuwahudumia Waafrika baada ya wao kuondoka.

Vilevile, jamii ya *Wimbo Mpya* ilikuwa chini ya utawala wa wakoloni Waingereza. Wakoloni hawa waliingia katika jamii hii na kuanza kupigana vita na watu weusi ili waweze kudhibiti na kuendeleza shughuli zilizokuwa zimewaleta huko. Ukoloni huu ulikuwa na athari zake katika jamii husika. Waafrika waligawanyika vikali. Kuna wale ambao walibakia kuwa wazalendo hadi mwisho wa ukoloni mkongwe huku wengine wakiwa wasaliti wakubwa.

#### 2.3.1.1.1 Athari za ukoloni mkongwe

Ukoloni mkongwe uliifanya jamii ya *Wimbo Mpya* kugawika katika makundi ya wazalendo na wasaliti.

##### 2.3.1.1.1.1 Uzalendo

Uzalendo ni ile hali ya mtu kuipenda na kuithamini nchi yake na kuweka maslahi ya taifa lake mbele na hivyo, kuwa tayari kulitumikia kila wakati. Mwandishi ameujenga uzalendo katika kazi husika kupitia kwa wapiganiaji uhuru walioongozwa na Meja Marete. Hili lilikuwa jeshi lililojiita "Jeshi la wazalendo." Kitendo cha kuziacha familia zao na kwenda kuishi msituni ili kuupigania uhuru wao kilikuwa dhihirisho kamili la uzalendo. Licha ya changamoto zote walizokumbana nazo msituni zikiwepo kukosa chakula na kulala kwenye baridi, azma yao ya kupigania uhuru kwa jamii yao haikufifia.

Kutokana na hali ya uzalendo, Meja Marete alimwacha mke wake aliyekuwa mgonjwa chini ya ulinzi wa majirani na kuendelea kuishi msituni kwani aliamini kuwa akirudi nyumbani kabla ya uhuru kupatikana, lengo lake la kupigania uhuru halitakuwa limetimia. Ugonjwa ulimzidia Nkirote na akafa huku Marete akiliendeleza azimio lake la uzalendo huko msituni. Aidha, ulaji viapo, uaminifu na uwekaji siri pamoja na kufuata sheria zote katika harakati za msituni na hata udumishaji nidhamu wa jeshi la wazalendo yalidhihirisha uzalendo wao.

Wananchi wengine kama Rogere walionyesha uzalendo wao hata ingawa hawakuwa wamejiunga na jeshi la vita. Aliwaunga mkono wapiganaji hawa kwa kuwapikia chakula walicholia huko kwake na hata cha kubeba huko msituni. Aidha, alikusanya habari zote zilizowasaidia wapiganaji weusi kukwepa mitego ya maadui.

**2.3.1.1.1.2 Usaliti**

Katika harakati za upiganiaji uhuru wa mataifa mengi barani Afrika, baadhi ya Waafrika waliwasaidia wakoloni kuwapiga vita Waafrika wenzao. Tendo hili lilidhihirisha usaliti mkubwa waliokuwa nao Waafrika kwa wenzao. Wengi wao walifanya hivi wakiwa na matumaini kuwa viongozi wa serikali za kikoloni wangewazawadi kwa kuwapa vyeo katika serikali zao. Ni kutokana na usaliti huu ambapo baadhi ya wasaliti hao walichaguliwa kuwa machifu walioshiriki katika matendo ya kuwadhulumu Waafrika wenzao.

Katika *Wimbo Mpya*, hali haikuwa tofauti. M' Keambati aliyekuwa Mwafrika alichaguliwa kuwa chifu wa kikoloni na kulisaidia jeshi la askari wa kikoloni kuwaangamiza Waafrika wenzake katika harakati za upiganiaji uhuru. M' Keambati aliwafichua Waafrika walioishi msituni kwa ajili ya kupigana vita vya uhuru na hata kuwaripoti wale ambao aliwatuhumu kuwa na uhusiano na wapiganiaji uhuru wa Kiafrika. M' Keambati kama msaliti aliongoza katika juhudi za kumsaka Meja Marete ambaye aliitwa haramia na wanamgambo wa kikoloni kwa sababu ya kuongoza vita vya kuwaondoa wabeberu katika jamii yao. Usaliti huu ulimfanya Nkirote, mkewe Marete kuota ndoto ya kutisha baada ya mumewe kuingia nyumbani usiku na kutoweka tena hadi msituni. Katika ndoto yake, alimwona mamake Kenoti akichapwa sana na kundi la wanamgambo lililoongozwa na M' Keambati huku akiambiwa atoe habari kumhusu mwanawe aliyekuwa amejiunga na jeshi la kivita la Meja Marete. Aidha, alimwona mumewe akishambuliwa kwa bunduki na wanamgambo. Punde tu alipogutuka kutoka usingizini, Nkirote alitishwa sana na ndoto yake na kushindwa kulala tena usiku kucha**.**

Ukoloni mkongwe pia ulikuwa na athari nyingine nyingi kando na swala la uzalendo na usaliti. Hizi zilikuwa kunyakuliwa kwa mashamba ya Waafrika, kudhulumiwa kwa kufanyishwa kazi ngumu na kuvurugwa kwa utamaduni wa watu weusi.

#### 2.3.1.2 Ukoloni mamboleo

Ukoloni mamboleo ni hali ya mataifa yaliyokuwa yamezitawala nchi za Kiafrika kuendelea kuzitawala nchi hizi kiuchumi na kisiasa hata baada ya wao kuondoka katika nchi hizi baada ya uhuru. Ukoloni mamboleo umekuwa tatizo sugu barani Afrika. Msingi wa ukoloni mamboleo uliwekwa na mabepari wakati wa ukoloni mkongwe. Kipindi chote cha ukoloni, wakoloni walisomba rasilimali zote za bara Afrika na kuzitumia kwa manufaa yao wenyewe.

Baada ya Vita vya Pili vya Ulimwengu ambapo Waafrika walilazimishwa kumpigania mkoloni, walianza kupata mwamko wa kisiasa. Katika miaka ya hamsini na sitini, Waafrika katika mataifa mengi walianza kupigania uhuru wao. Hatimaye hata mataifa ya Afrika Mashariki yalijinyakulia uhuru wao.

Hatimaye ukoloni mamboleo ulichipuka na ukawa mfumo rasmi wa kuendelea kuzinyonya rasilimali za bara Afrika kwa njia rahisi ya kutoa misaada inayoambatana na masharti magumu yanayodumisha umaskini wa bara hili. Ukoloni mamboleo huendelezwa kupitia taasisi za kimataifa na mashirika ya kimataifa ambayo hushirikiana kuyawekea mataifa machanga vikwazo vya kimaendeleo.

### 2.3.2 Ukosefu wa elimu

Elimu ni chombo muhimu cha kuendeleza matabaka katika jamii. Hali hii ndiyo inayosababisha mikinzano ya kitabaka ambayo ameizungumzia Marx katika nadharia yake. Elimu ni mojawapo ya vigezo vilivyotumiwa na watawala wa kikoloni ili kumtenga Mwafrika na kuhakikisha kuwa amebaki katika hali duni. Hii ni kwa sababu watu wachache waliokuwa wamesoma walikuwa na nafasi bora za kupata kazi, hivyo basi kujiinua kiuchumi. Wakati wa ukoloni, Waafrika wachache sana walihudhuria elimu hasa ya madarasani. Waliobahatika kupata fursa ya kuelimika walikuwa vibaraka vya wakoloni. Kwa sababu hii, idadi ya Waafrika waliopata elimu ilikuwa ndogo ikilinganishwa na ile ya wakoloni.

Wengi wa Waafrika pia hawakujua thamani ya elimu na kwa hivyo, hawakuona haja ya kuingia shuleni. Aidha, shule zilikuwa chache na waliopewa kipaumbele katika shule hizi walikuwa ni Wazungu, bali sio Waafrika. Changamoto nyingine ni kuwa shule hizi zilikuwa mbali kiasi cha

kutoweza kufikika kwa urahisi. Aidha, zilikuwa katika sehemu chache ambazo wakoloni walikuwa wakiishi na ambapo walikuwa na misheni.

Katika jamii ya *Wimbo Mpya*, hali ilikuwa hiyo hiyo na hata baada ya uhuru, elimu ilikuwa changamoto kubwa. Katika riwaya hii, tunaelezwa kuwa kwenda shule mfululizo halikuwa jambo la kawaida. Aidha, watoto wengi walienda shule miezi michache kisha wakawa wanakatiza na kurudi tena baada ya wiki kadhaa au hata miezi. Wengine wao pia tumeelezwa kuwa waliamua kuwa shule zilikuwa ni upuzi mtupu na wakaacha kabisa, huku wengine wakiwa hawakukaribia milango ya shule. Isitoshe, umuhimu wa shule haukuwa umetambuliwa na wengi huko mashambani huku shule nazo zikiwa chache. Nao watoto kutoka vijiji vilivyozunguka mji wa Tanta walitembea mwendo mrefu kuhudhuria shule mjini humo. Vilevile, kulikuwa hakuna shule vijijini.

### 2.3.3 Dhuluma dhidi ya wanawake

Katika jamii nyingi barani Afrika, mwanamke amekuwa akidhulumiwa aghalabu kutokana na mila zinazomtambua mwanamume huku kwa upande mwingine zikimkandamiza mwanamke. Kulingana na utafiti wa Murungi (2013), mwanamke amedunishwa na kudhulumiwa kulingana na mila ambazo hazimpi nafasi katika jamii.Ni kutokana na mila hizi potovu ambapo mhusika Natala katika tamthilia ya *Natala* anajitokeza na kupigania haki zake na hivyo basi, kuwa kielelezo cha wanawake cha kupigania haki zao na kwa njia hii, kujiepusha na dhuluma wanazotendewa katika jamii. Aidha, utafiti wa Chacha (2013) umebainisha kuwa mwanamke katika jamii hudhulumiwa kutokana na asasi mbalimbali katika jamii wanamoishi wanawake. Asasi hizi ni ndoa, dini na mila na desturi za jamii husika. Ni kutokana na asasi ya dini ambapo Mwavita kama mwanamke katika tamthilia ya *Mama ee* anadhulumiwa kwa kuambiwa na padre kuwa hafai kuachana na mumewe hata shida zinapoingia katika ndoa yao. Tayari, mumewe Kinaya alimtesa katika ndoa yao kwa kufuata mila na desturi za jamii yao.

Kulingana na Njogu na Wafula (2007), Nadharia ya Ufeministi inaonyesha kuwa mwanamke amekuwa akidhulumiwa katika jamii kwa muda mrefu. Nia ya wahakiki wa nadharia hii ilikuwa kuangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa shida zinazowakabili wanawake

zimejengeka kwenye misingi ya jinsia yao. Haya ni maelezo yanayodhihirisha kuwa mwanamke anadhulumiwa katika jamii na ni kutokana na dhuluma hizi ambapo aina nyingi za Ufeministi zilizuka ili kupigania haki za wanawake wanaodhulumiwa katika jamii mbalimbali.

Katika *Wimbo Mpya,* changamoto ya dhuluma dhidi ya wanawake imeendelezwa kupitia kwa ndoa kati ya Bi. Mariamu na Ezra Thuranera kabla ya kutalakiana. Katika maisha yao ya ndoa, Bi. Mariamu hakufanikiwa kupata mtoto. Kutokana na jambo hili, Ezra alimdhulumu mkewe kwa kwenda kupata watoto nje ya ndoa bila ya idhini yake na kuwaleta watoto hao kwa mkewe ili aje kuwalea. Bi. Mariamu aliyavumilia haya yote na kuendelea kuishi na mumewe huku akiwa angali anampenda licha ya maovu haya.

Ezra pia alipiga hatua zaidi na kumchumbia mwanamke mwingine ambaye walikuwa wamepanga kuoana. Katika utasa wake, Bi. Mariamu hakulipinga wazo la mumewe na alikuwa tayari kuishi vizuri na mke mwenza. Ajabu ni kuwa mchumba wake Ezra alimwambia kuwa yeye hakuwa tayari kuishi na mwanamke mwingine. Kwa hivyo, mwanamke huyu alimshinikiza mchumba wake Ezra amfukuze Bi. Mariamu kabla ya wao kuoana. Jambo hili lilitimizwa huku Bi. Mariamu akizidi kudhulumiwa kwa sababu ya utasa wake. Bi. Mariamu aliondoka huku akivumilia uchungu wa kumpoteza mume wake aliyempenda.

Kakake Bi. Mariamu kwa jina Yohana Nthambori alishiriki katika kumdhulumu dadake. Baada ya kutalakiana na mumewe, Bi. Mariamu alienda kuishi kijijini katika nyumba ya marehemu babake. Nyumba hii ilikuwa imezingirwa na shamba kubwa. Kwa kufuata mila na desturi za jamii ambazo hazikumruhusu mwanamke kurithi chochote, Nthambori alimkandamiza dada yake kwa kutomrithisha mali yoyote bila kutia maanani kuwa Bi. Mariamu ndiye aliyekuwa akiishi katika nyumba hii kama mgeni ambaye hakutangamana na wanakijiji wowote. Kwa sababu ya dhuluma hii, ilimbidi aache mazao shambani bila kutumiwa na yeyote kwa kuwa kakake aliishi mjini na kwenda kununua alichohitaji kutoka kwa jirani yake. Baadaye, Nthambori alimdhulumu dadake tena kwa kumfukuza kutoka kwa nyumba ya babake na kuwaagiza wafanyikazi wake wavitupe vitu vyake vyote nje. Baada ya kufanya hivi, aliifunga nyumba na kuondoka. Nthambori alidai alifanya hivi kwa kuwa dada yake aliifedhehesha familia yao kwa kwenda kuishi kijijini na kutangamana na watu maskini.

Utafiti uliofanywa na Padri Mario kwa muda wa miaka mitano kuhusu mila na utamaduni wa Wameru ulibainisha kuwa jamii iliwabagua na kuwadhulumu wanawake. Katika mazungumzo yake na Mwathi, Padri Mario alisema:

> Nina ushahidi wa kutosha wa kuonyesha kwamba jamii yenu inawawabagua wanawake na kuwakandamiza. Mnawapiga, mnawafungia jikoni na kuwafanyia kila aina ya dhuluma… Ithibati muhimu zaidi niliyo nayo ni ya kwamba mnawathamini na kuwapendelea watoto wa kiume kuliko wale wa kike. (uk. 51).

Maelezo haya ni ithibati tosha kuwa mwanamke alikuwa akidunishwa na kudhulumiwa katika jamii ya *Wimbo Mpya*.

### 2.3.4 Utabaka

Katika jamii nyingi barani Afrika, utabaka umesheheni. Kwa mujibu ya Nadharia ya U-Marx katika Wamitila ( 2006: 183), historia ya maisha ya binadamu ni harakati za kitabaka. Hatua ya juu ya mwendeleo wa utabaka ni uzukaji wa mfumo wa ubepari ambapo mali humilikiwa na watu wachache. Kauli hii inaonyesha hali halisi katika jamii za leo ambapo mali humilikiwa na matajiri ambao ni wa tabaka la juu. Tabaka hili aghalabu ndilo hujumuisha viongozi wa nchi. Tabaka la chini nalo huwa la wanyonge ambao huendeleza maisha yao kutokana na ujira mdogo wanaoupata kutokana na kufanya kazi kwa matajiri wa tabaka la juu.

Katika kazi hii, jamii ya *Wimbo Mpya* imekumbwa na changamoto ya utabaka. Kuna matabaka ya mabwanyenye na wanyonge, walio na elimu na wasio na elimu. Tabaka la mabwanyenye linawakilishwa na watu kama Yohana Nthambori. Huyu alikuwa mwana wa M' Keambati, mmoja wa machifu wa kikoloni na aliyekuwa tajiri mkubwa. Yohana alifanya kazi mjini kama hakimu mkuu. Kutokana na cheo chake cha juu serikalini, alijiona kama mtu ambaye hakufaa kutangamana na watu maskini vijijini. Alikitembelea kijiji alikozaliwa mara chache sana kwa ajili ya kwenda kuliangalia shamba lake la mibuni ambalo lilikuwa likitunzwa na wafanyikazi wake wa tabaka la chini.

M’ Keambati pia alikuwa mtu wa tabaka la juu kabla ya kifo chake. Watoto wake walisomea mjini Tanta na hata waliporudi nyumbani, hawakuenda kucheza na watoto wengine kijijini. Hii ilikuwa ishara ya utabaka.

Tabaka la chini nalo linawakilishwa na wanakijiji wa kawaida kama vile Getimbo, Rogere, Marete na wengineo. Kwa upande mwingine tabaka la wenye elimu linawakilishwa na Bi. Mariamu ambaye ana ndoto kuu ya kukiendeleza kijiji chake kama kielelezo cha mtu mwenye elimu na aliyewajali wanajamii. Walimu wenzake, Esta na Sara walikuwa katika tabaka la wenye elimu.

Tabaka la wasio na elimu linawakilishwa tena na wanakijiji wa kawaida ambao hawakubahatika kupata masomo. Watu hawa pia ndio wanaowakilisha tabaka la chini. Hii ina maana kuwa elimu humsaidia sana mtu katika kupaa juu kitabaka. Rogere ambaye alijiona kuwa mtu ambaye hangeweza kusaidia lolote katika ujenzi wa shule kwa sababu ya ukosefu wa elimu yumo kwenye tabaka hili.

### 2.3.5 Mvutano baina ya usasa na ukale

Jamii nyingi hasa za Ulimwengu wa Tatu zimetawaliwa na dhana kuwa usasa ulioachwa na Wazungu baada ya uhuru na unaozidi kuenezwa hadi wa leo una manufaa kwa jamii hizi. Baada ya wakoloni kuondoka, Waafrika walianza kuziacha mila zao na kuiga mila za Wazungu. Hili ni jambo linaloendelea hata katika jamii za leo. Baadhi ya mila hizi zikiwepo uigaji wa mitindo ya mavazi ya Wazungu hazivutii. Kwa upande mwingine kuna wazee katika jamii ambao hawavutiwi na mila hizi na wanaziona kuwa potovu. Wanashikilia kuwa mila na tamaduni zao za Kiafrika ndizo bora zaidi. Kutokana na mitazamo hii tofauti baina ya vijana na wazee, mvutano umezuka katika jamii nyingi kuhusiana na jambo hili.

Katika riwaya husika, kuna mvutano baina ya ukale na usasa kupitia kwa mazungumzo ya Mwathi na Yohana Nthambori. Yohana anapomtembelea Mwathi kijijini, mzee huyu anamwandalia mgeni wake pombe ya kienyeji wanayoendelea kunywa katika harakati za Yohana kumweleza mwenyeji wake sababu yake ya kumtembelea. Kulingana na mazungumzo yao, Yohana anaonelea kuwa pombe kama hiyo haikuweza kudumu kwa muda mrefu bila

kuharibika. Kwa hivyo, anapendekeza pombe ya kisasa ya chupa ambayo ingeweza kudumu kwa muda mrefu.

Kulingana na Mwathi, pombe ya kienyeji ilikuwa bora kuliko ile ya kisasa.  Kwa sababu hii, aliwataka wale wenye elimu ya Mzungu kama Yohana Nthambori wajipatie maarifa ya kuvifanya vitu vyao kama vile pombe ya kienyeji kukaa kwa muda mrefu bila kuharibika. Ukweli ni kuwa Nthambori aliipenda sana pombe ya kienyeji ya mwenyeji wake lakini hakutaka Mwathi atambue kuwa aliithamini huku akiwa wa tabaka la juu lililojihusisha na vitu vya kisasa. Kwa sababu hii, Nthambori aliondoka na kwenda kunywa bia huko mjini Tanta kwenye baa la kisasa na la tabaka lake.

Kutokana na changamoto tulizozielezea katika kazi hii, Jamii ya *Wimbo Mpya* ilihitaji kujikomboa dhidi ya baadhi ya changamoto zilizoikumba jamii hii.

### 2.4 Aina za ukombozi katika *Wimbo Mpya*

Katika riwaya husika, kuna aina tofauti za ukombozi ambazo tutazishughulikia katika kazi yetu. Aina za ukombozi zinazojitokeza katika jamii hii ni ukombozi wa kisiasa, ukombozi wa kielimu na ukombozi wa kiuchumi**.**

#### 2.4.1 Ukombozi wa kisiasa

Ukombozi wa kisiasa ni hali ambapo taifa au hata jamii hujaribu kujinasua kutokana na minyororo ya ukoloni hasa kupitia kupigana vita na wakoloni. Katika *Wimbo Mpya*, kuna aina mbili za ukombozi wa kisiasa ambazo ni ukombozi wa kisiasa kabla ya uhuru na ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru.

##### 2.4.1.1 Harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe

Katika mataifa mengi barani Afrika, harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe ziliendelezwa kupitia kupigana vita na wakoloni waliokuwa wamenyakua sehemu mbalimbali kwa manufaa yao wenyewe. Huu ulikuwa ukombozi uliohusisha umwagikaji wa damu ili Mwafrika aweze kuwa huru. Vita hivi havikuwa rahisi kwa kuwa Waafrika wengi hawakuwa na

ushirikiano katika juhudi zao za kumwondoa Mzungu na pia silaha zao zilikuwa duni zikilinganishwa na zile za wakoloni.

Katika kazi husika, mwandishi ameuendeleza ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe kupitia kwa vita kati ya wakoloni Waingereza na Waafrika. Vita vya kupigania uhuru viliongozwa na Meja Marete ambaye aliliongoza kundi lake la vita kwa jina jeshi la wazalendo. Ukombozi huu ulihusisha mapigano mbalimbali ambapo mwanzoni jeshi la wazalendo lilionekana kufaulu kwa kiasi kikubwa. Ufanisi huu ulitokana na juhudi za wapiganaji wa jeshi la Marete kuwanyang'anya wapiganaji wa jeshi la kikoloni silaha zao bora zikiwepo bunduki za kisasa baada ya kuwashambulia na kuwaua wengi wao. Baadaye, jeshi la askari wa kikoloni lililipiza kisasa ili kuonyesha umaarufu na uthibiti wao dhidi ya watu weusi.

Hata hivyo, Waafrika hawakufa moyo. Waliendelea na juhudi zao za kujikomboa huku wakiishi msituni katika kambi ambazo hazikuwa na majengo yoyote. Juhudi hizi za ukombozi zilisababisha vifo vingi vya Waafrika na hata wakoloni wenyewe. Kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe hakukuwa jambo rahisi kwani watu kama Meja Marete walishiriki katika vita vya ukombozi huku hali za familia zao zikiwa duni. Alikuwa amemwacha mkewe akiwa mgonjwa sana na hata hakuwa na yeyote wa kumhudumia. Jambo hili pia lilimtia wasiwasi na huzuni nyingi mkewe na hata watoto wake kwani hawakujua ni lini baba yao angerudi nyumbani na kuishi na wao.

Kutangazwa kwa hali ya hatari Januari mwaka wa 1952 kuliifanya hali ya vita vya ukombozi izidi kuwa ngumu zaidi. Kutokana na hali hii, hakuna mtu aliyeruhusiwa kutoka nje, kwa hivyo watu kama Meja Marete na jeshi lake walikuwa katika hatari kubwa ya kukamatwa na wamamgambo wa kikoloni na hata kuuawa kwa kosa la kuishi msituni. Hata kabla ya hali ya hatari kutangazwa, Marete alikuwa akisakwa usiku na mchana na wanamgambo hao kwa kosa la kuongoza vita vya kuwakomboa Waafrika wenzake kutokana na hali ya ukoloni. Kwa hivyo, usalama wake ulikuwa hatarini maradufu.

Harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni mkongwe ziliendelea hadi mwaka wa 1963 ambapo uhuru ulipatikana na taifa jipya likazaliwa. Wimbo wa mapambano dhidi ya wakoloni ulifikia

kikomo wakati huu. Uhuru wenyewe ulipokelewa kwa mitazamo tofautitofauti na wanajamii mbalimbali.

Mtu kama Mwathi alionelea kuwa uhuru haukuyabadilisha maisha yake kwa kiasi kikubwa kwani aliendelea na shughuli zake za kawaida kila siku baada ya uhuru. Kwa upande mwingine, baadhi ya wapiganiaji uhuru walidai kuwa hawakupata uhuru kamili na kwa sababu hii waliamua kusalia msituni hadi uhuru kamili upatikane. Hii ilikuwa ishara ya uongozi mbaya. Hisia hizi mbalimbali ndizo zilizopelekea kuanza kwa ukombozi wa pili dhidi ya ukoloni mamboleo punde tu baada ya uhuru.

### 2.4.1.2 Ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru

Mapambano dhidi ya utawala mbaya yaliendelea hata baada ya uhuru wa kisiasa kwa kuwa Waafrika wengi waligundua kuwa uongozi wa viongozi waliochukua hatamu baada ya uhuru haukuwa tofauti sana na ule wa wakoloni walioondoka. Aidha, walikuja kuelewa kuwa ulikuwa uhuru wa bendera tu. Kwa mujibu wa mihimili ya nadharia ya U-Marx katika Wamitila (2006: 182- 184), nadharia ya U-Marx inapaswa kuhusishwa na kuandamana pamoja na hata kuelekeza kwa matendo ya kiutekelezaji dhidi ya mfumo mzima wa ubepari. Kuhusiana na hili, mataifa mengi barani Afrika yalijiingiza katika juhudi za kupigana na ukoloni mamboleo ili kuuvunjilia mbali mfumo wa utawala mbaya uliokuwa umeenea katika mataifa haya. Ukombozi huu unaendelea hadi wa leo katika mataifa mengi ya Ulimwengu wa Tatu.

Baada ya uhuru, jamii ya *Wimbo Mpya* haikushuhudia mabadiliko iliyoyatarajia kutokana na kupatikana kwa uhuru. Ukoloni mamboleo ulianza kumea mizizi, hivyo basi jamii hii ikaanza kupigana ili kujikomboa. Kunyakuliwa kwa ardhi ya baadhi ya wanajamii na kukosa kurudishiwa ardhi yenyewe ndicho kilikuwa hasa kiini cha ukombozi wa pili. Ukombozi huu ulianzia kwa baadhi ya wapiganiaji uhuru akiwepo Meja Marete kuamua kubaki msituni na kuendelea na vita hadi pale ambapo serikali mpya ingetimiza ahadi zao za baada ya uhuru na uhuru wa kweli kupatikana. Meja Marete ndiye aliyekuwa katika mstari wa mbele wa kuzingatia jambo hili. Kulingana naye, uhuru haukuyabadilisha maisha yake. Aidha, alikuwa katika kikundi cha wapiganiaji uhuru kilichodai kuwa serikali mpya ilikuwa ya mahaini na hivyo basi,

hawakuitambua. Marete aliendelea kudai kuwa masetla walifaa kuirudisha ardhi yao waliyokuwa wameitwaa ili waweze kuwa na uhuru kamili.

Kundi la Marete sio tu la pekee lililobaki msituni. Kulikuwa na makundi mengine yaliyobaki huko ingawa baadhi ya wanamakundi haya walitii sheria ya serikali mpya ya kuwaagiza wapiganiaji uhuru waliokuwa wamesalia msituni kurudi nyumbani na kwenda kuyaanza maisha mapya. Waliosalia msituni waliendelea na harakati zao za ukombozi. Mara kwa mara waliyashambulia maboma ya masetla walioachwa nchini baada ya wenzao kuondoka na hata kuwaibia mifugo wao.

Haya yalifanywa kwa imani kwamba masetla hawa wangeondoka na kuiacha ardhi yao. Juhudi hizi ziliendelea hadi wakati ambapo ujumbe kutoka kijijini uliojumuisha Rogere, Getimbo, Igweta na Bi. Mariamu, aliyekuwa mwanamke wa pekee katika kundi hilo, ulifika msituni alikoishi Marete. Marete alishangaaa kwa kuwa hakuelewa ni vipi kundi hili lilitambua mahali walimokuwa msituni.

Aidha, alizidi kushangazwa na juhudi za mwanamke wa pekee kutembea mwendo mrefu hivyo msituni. Lengo kuu la wanakijiji hawa lilikuwa kwenda kumsihi Marete kurudi nyumbani kutoka na hali mbaya ya ugonjwa wa mkewe ambaye wakati huu alikuwa amelazwa hospitalini. Baada ya kupashwa ujumbe huu, Marete alibakia bila lingine la kufanya ila tu kurudi nyumbani kutokana na roho ya utu ili kwenda kumshughulikia mke wake aliyekuwa mgonjwa.

Huu ndio uliokuwa mwisho wa mapambano dhidi ya utawala mbaya baada ya uhuru kwa kuwa baada ya Marete kukubali kurudi nyumbani, wenzake waliamua kutawanyika na kurudi makwao. Wakati huu, wapiganaji wote waliokuwa wamebakia msituni walikuwa wamekusanyika katika kambi moja, kwa hivyo, hakuna yeyote aliyebaki msituni. Wote waliuaga msitu na kwenda kuungana na wanajamii wenzao katika kuimba "Wimbo Mpya" wa baada ya uhuru wa harambee, uhuru na kazi.

Marete na kundi lake walipofika nyumbani, walipata kuwa bibi yake alikuwa ameaga dunia siku iliyotangulia. Mipango ya mazishi iliandaliwa na baada ya mazishi, Marete alijiunga na

wanajamii wenzake katika kuuimba "Wimbo Mpya" ambao haukuzaa matunda mengi kwa wanajamii kama walivyotarajia baada ya uhuru.

### 2.4.2 Ukombozi wa kielimu

Katika *Wimbo Mpya*, mwandishi ameuendeleza ukombozi wa kielimu kupitia kwa mhusika mwanamke kwa jina Bi. Mariamu. Mwanamke huyu amesawiriwa kama kielelezo katika kuikomboa jamii kielimu na hivyo basi kuitambua nafasi ya mwanamke katika ukombozi wa kielimu**.**

#### 2.4.2.1 Nafasi ya wanawake katika ukombozi wa kielimu

Nchini Kenya na hata ulimwenguni kote, wanawake wamekuwa wakichukua nafasi kuu katika kuikomboa jamii katika nyanja mbalimbali zikiwepo za elimu, siasa, mazingira na nyinginezo. Michelle Bachelelet, ambaye ndiye rais wa nchi ya Chile, alianzisha mfumo wa mabadiliko ya kielimu ambao uliinua kiwango cha uwekezaji wa serikali katika elimu ya umma mwaka wa 2014. Kiongozi huyu wa kike pia alifadhili mpango wa usawa wa jinsia unaowapa haki sawa za elimu bora watoto wa kike na wa kiume. Michelle pia ameonyesha umuhimu wa kushughulikia elimu ya mtoto msichana kwa kusema kuwa wasichana wanapoelimika, elimu hiyo huwaweka katika njia ya kujiinua na kufikia viwango vya juu vya kiuchumi na kushiriki katika maendeleo ya jamii.

Katika riwaya husika, mwandishi amemtumia Bi. Mariamu kama kielelezo na daraja la kuwavusha wanajamii kutoka kipindi cha ukoloni hadi kipindi cha baada ya uhuru kwa kuwashirikisha wanajamii katika ujenzi wa taifa baada ya uhuru kwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa shule. Lengo kuu la Bi. Mariamu lilikuwa kuwashirikisha wananchi katika kuuimba "Wimbo Mpya" wa harambeee, uhuru na kazi. Alitaka pia kuwazindua wananchi katika kuelewa kuwa ujenzi wa taifa baada ya uhuru haukuwa jukumu la serikali peke yake, bali lilikuwa jukumu la serikali ikisaidiana na wananchi wake.

Bi. Mariamu amechorwa kama mwanamke mwenye fikira za juu hata kuliko mwanamume yeyote kijijini alimoishi. Wazo la kuanzisha mradi wa kujenga shule lilimjia Bi. Mariamu

aliporudi kijijini alikozaliwa baada ya kutalakiana na mumewe. Mwanamke huyu pia aliona shida ya ukosefu wa elimu iliyowakumba wanajamii.

Baada ya kutangamana na wanakijiji wachache, Bi. Mariamu alikuja kujuana na Mwathi aliyemiliki ardhi kubwa. Mwanamke huyu alimshirikisha Mwathi katika mradi wake wa ujenzi wa shule kwa kuenda kwake ili akamwombe kipande cha ardhi cha kujengea shule. Mwanzoni, Mwathi alishangazwa na mwanamke huyu kwani hakuona jambo lolote waliloweza kuzungumzia kwa sababu ya tofauti za umri na za kitabaka kati yao. Aidha, alikuwa haelewi ni nini alichozungumzia mwanamke huyo. Bi. Mariamu alipogundua kuwa mzee huyu hakumwelewa, alienda moja kwa moja na kumwambia: "Mzee, nimekuja kukuona ili kukuomba uchangie kwenye mradi wa kujenga shule hapa kijijini" (uk. 33).

Maneno haya yalimshangaza Mwathi sana kwa kuwa hakuelewa ni vipi ambavyo mzee kama yeye angechangia katika ujenzi wa shule. Pia alizidi kushangaa ni vipi mwanamke kama huyo angejishirikisha na mambo makubwa kama ujenzi wa shule. Bi. Mariamu alimfafanulia zaidi na kumwambia kuwa alitaka awagawie kiwanja cha takribani ekari mbili cha kujengea shule. Mwathi alimwambia mwanamke huyu kwamba alikuwa tayari kutoa kiwanja.

Hatua iliyofuata kuhusiana na mradi wa Bi. Mariamu ilikuwa kuwaita waalimu wenzake, Esta na Sara ili waje kulizungumzia jambo hilo ndipo ayasikie maoni yao. Walimu hawa walikuwa na hisia tofauti kuhusiana na mradi huu. Kulingana na Sara na Esta, jukumu la ujenzi wa shule lilikuwa la serikali, bali sio la wananchi. Bi. Mariamu kwa upande wake aliwahamasisha kuwa jukumu hili lilikuwa la serikali ikishirikiana na wananchi. Mwanamke huyu pia aliwaelezea marafiki zake kuhusu hatua aliyokuwa ameipiga ya kupata uwanja wa ujenzi wa shule hii. Esta na Sara walimchukulia Bi. Mariamu kama mwanamke asiye wa kawaida kutokana na kazi aliyokuwa ameifanya. Hao wawili walikubaliana kuwa huyo alikuwa Bi. Mariamu mpya na mwenye mawazo ya kiuanaume.

Bi. Mariamu alimshirikisha mwanakijiji Rogere katika mpango wake wa ujenzi wa shule. Alipomtembelea kwake, alimfichulia sababu yake ya kumtembelea na kusema : "Nataka tujenge

shule ya msingi hapa kjijini kwa manufaa yetu sote. Ili kufanikisha mradi huu, itabidi tushirikiane. Kila mmoja wetu atoe mchango fulani…" (uk.71).

Maneno haya yalimfanya Rogere acheke kwani kulingana naye, ujenzi wa shule ulikuwa wa watu wenye elimu. Bi. Mariamu alimkosoa Rogere kwa kumfahamisha kuwa kila mtu alikuwa na jukumu lake katika kuleta maendeleo. Rogere hakuchelea kutoa mchango wake. Alimwahidi mwanamke huyu kuwa angetoa mbao zote zilizohitajika katika ujenzi wa shule. Aidha, Rogere alimhakikishia Bi. Mariamu kuwa angemsaidia katika kulisambaza wazo la ujenzi wa shule kwa wanakijiji kwa kuwa mwanamke huyu alikuwa bado mgeni kijijini na alikuwa bado hajazoeana na wengi wa wanakijiji hao.

Rogere anaanza kutimiza ahadi yake ya kusambaza habari juu ya ujenzi wa shule bila kukawia. Anamtembelea jirani yake Getimbo na kumpasha habari hizi pamoja na juhudi zote alizokuwa amezifanya Bi. Mariamu kuhusiana na mradi wa ujenzi wa shule. Getimbo analionelea wazo la Bi. Mariamu kuwa la kuwatawala wanaume lakini Rogere anamwelezea kuwa hilo lilikuwa tendo la ushirikiano kati ya wanakijij na Mwanamke huyo. Hatimaye, Getimbo anaunga mkono mradi huo kwa kuahidi kutoa nusu ya mabati yote yaliyohitajika. Ukakamavu wa Bi. Mariamu unamfanya Getimbo afikirie kuwa dunia ilikuwa imebadilika.

Vifaa vyote vya ujenzi vinapokusanywa, wanakijiji wanajumuika na kuitikia wito wa harambee katika kushirikiana kwenye ujenzi wa shule ya msingi ya Gaito. Ujenzi wa shule unapokamilika, wanakijiji wanayapokea maendeleo haya kwa kuandaa karamu na baada ya kula, wanafurahia juhudi na ushindi wao kwa wimbo kwa kuuashiria Wimbo Mpya wa baada ya uhuru. Wimbo huu uliongozwa na Marete aliyekuwa mzalendo katika kulikomboa taifa kutokana na ukoloni. Wimbo huu ulisema:

**Marete:** Wimbo mpya wa Kenya unasema
**Wote:** Uhuru na kazi
Harambee na maendeleo
Tupigane na magonjwa
Tupigane na ujinga
Tupigane na umaskini…( uk. 82)

Wimbo huu unaonyesha juhudi za wananchi za kuamua kujishirikisha katika kulijenga na kuliendeleza taifa lao baada ya uhuru.

Baada ya ujenzi wa shule kukamilika kabisa, kamati ya shule inachaguliwa ikiongozwa na Marete kama mwenyekiti wao. Shule ya Msingi ya Gaito inasajiliwa na kutambuliwa rasmi na wizara ya elimu. Aidha, inaanza kupokea walimu kutoka kwa wizara ya elimu na hata Bi. Mariamu kama mwalimu na mwanzilishi wa shule yenyewe anapata uhamisho na kuja kufunza katika shule hii. Wanakijiji nao wanaanza kuhamishia watoto katika shule yao waliyoshiriki katika kuijenga na iliyokuwa karibu.

Mwandishi amemchora Bi. Mariamu kama mwanamke aliye na ufanisi mkubwa katika kuendeleza elimu kijijini. Uwezo alio nao sio wa kawaida kwani yeyote aliyemwendea ili kuomba usaidizi wa ujenzi wa shule ya msingi ya Gaito, hakumkatalia mwanake huyu. Wanakijiji wote walitoa michango yao yote kwa moyo mkunjufu. Hili si jambo la kawaida kwa watu wengi, hata viongozi maarufu nchini.

**2.4.3 Ukombozi wa kiuchumi**

Maendeleo yoyote katika nchi hutegemea hali ya kiuchumi ya nchi husika. Kwa mujibu wa nadharia ya U-Marx katika Wamitila (2006:182-184), historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo itachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi na pia huathiri uzalishaji mali na usambazaji wa mali hizo. Iwapo uchumi wa nchi umeimarika, maendeleo mengi hupatikana katika nchi hiyo kinyume na uchumi uliozorota ambao hufanya maendeleo ya nchi kudidimia. Wawekezaji pia hupendelea kuwekeza katika nchi ambazo zina uchumi ulioimarika.

Mwandishi wa *Wimbo Mpya* amemtumia Bi. Mariamu kama kielelezo cha jamii katika ukombozi wa kiuchumi wa jamii husika. Ili uchumi wowote uweze kukua, uongozi imara wa makundi mbalimbali ya uwekezaji huwa jambo muhimu. Bi. Mariamu kama kiongozi wa kutegemewa analiongoza kundi la akina mama kutoka kijiji cha Gaito na vijiji vingine kama mwenyekiti waliyemchagua ili kujiendeleza kiuchumi. Kujengwa kwa shule ya msingi ya Gaito kulikuwa kama daraja la kuwaendeleza akina mama kiuchumi kwani baada ya ujenzi wa shule, walipata mahali pa kukutania ili waweze kupanga miradi yao ya kimaendeleo.

Kikundi hiki cha akina mama kilikutana kila siku ya Ijumaa katika shule hii. Lengo lao kuu lilikuwa ni kuchangisha pesa na kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile kushona viondo, kufuga nguruwe na kununua vinu vya kusagia unga. Kutokana na maendeleo ya kikundi hiki, idadi ya wanachama iliongezeka kila uchao. Akina mama hawa pia walikuwa na maono makubwa ya kufikia viwango vya juu zaidi kiuchumi kwani walikuwa na akaunti ya benki mjini Tanta na iliyokuwa na shilingi elfu hamsini. Hii ni hali inayopatikana katika vikundi vingi vya akina mama ambao huwa na ndoto ya kujiendeleza kiuchumi. Fedha kama hizi hutumiwa katika kuendeleza miradi mingi ya maendeleo ili kuinua uchumi wao binafsi na hata wa taifa nzima.

Kutokana na kipawa cha Bi. Mariamu cha uongozi mzuri, umaarufu wake ulienea kuanzia vijijini hadi kiwango cha kitaifa na hata bungeni. Hii ni changamoto kubwa kwa wanawake viongozi ili waweze kuuiga mfano huu ndio waweze kupata ufanisi kutokana na uongozi wao.

**2.5 Hitimisho**

Kwa wanajamii wa *Wimbo Mpya*, uhuru ulikosa kuwa na faida waliyoitarajia baadhi ya viongozi. Wao walishiriki ukatili na hata ubaguzi. Mwelekeo huu uliwafanya kuungana na wakoloni waliokuwa na tabia kama hizi. Aidha, wanajamii hawa walikuja kugundua kuwa "Wimbo Mpya" haukuwafaidi kwa kuwa hali yao ya maisha haikuwa tofauti sana na ile ya kabla ya uhuru. Baada ya uhuru, wapiganiaji uhuru walikuwa na matumaini makubwa kuwa ardhi yao ambayo ilikuwa imetwaliwa na wakoloni ingerudishwa lakini hili halikuafikiwa. Hii ilikuwa ishara kamili ya ukatili wa wakoloni. Aidha, wapiganiaji uhuru hao walikuwa wameahidiwa kuwa wakitoka msituni, wangesaidiwa kujenga upya maisha yao. Jambo hili halikutimizwa hata kamwe.

Vile vile, wakoloni hawa waliwatenga baadhi ya wapiganiaji wa uhuru badala ya kuwashirikisha kikamilifu katika shughuli za kitaifa. Jambo hili liliwavunja moyo na kuwafanya kuona kuwa juhudi zao za kumuondoa mkoloni hazikuwafaidi.

Aidha, ni kutokana na ukatili huu ambapo nyumba ya Marete ilichomwa, ardhi yake ikatwaliwa na wakoloni na familia yake kubaki bila makao. Jambo hili lilimtwika Rogere jukumu kubwa la

kuitunza familia yake na ya rafiki yake Marete kwa kuwa alikuwa hajatoka msituni hata baada ya uhuru.

Kitendo cha Yohana Nthambori cha kuwa na tamaa kubwa ya kumiliki sehemu kubwa ya ardhi kilikuwa zao la ukatili. Nthambori alikuwa mmoja wa Waafrika waliobahatika kupata elimu katika kipindi cha ukoloni mkongwe. Kutokana na elimu yake, alikuwa mmoja wa wale ambao walijaza nyadhifa za uongozi wa nchi kutoka kwa wakoloni baada ya wao kuondoka. Kama hakimu mkuu katika serikali mpya ya Waafrika, aliiga tabia za viongozi wa kikoloni waliokuwa na tamaa kubwa ya kumiliki ardhi kubwa. Hii ndiyo sababu iliyomfanya arudi kijijini na kujaribu kumshawishi Mwathi amuuzie kipande cha ardhi yake licha ya kuwa na ardhi kubwa aliyoirithi kutoka kwa baba yake, aliyekuwa chifu wa kikoloni, baada ya kifo chake.

Wazo hili lilimjia Nthambori baada ya kufikiwa na habari kuwa Mwathi alikuwa amemgawia dada yake kipande cha ardhi kwa ajili ya kujenga shule. Mwanamume huyu alimtishia Mwathi kwa kumwambia kuwa jukumu la ujenzi wa shule lilikuwa la serikali na kama angehalalisha shule ijengwe katika ardhi yake, kulikuwa na uwezekano mkubwa wa dola kunyakua uwanja zaidi kwa upanuzi wa mradi huu. Ukweli ni kuwa haya yalikuwa maneno tu ya kumtishia Mwathi amwuzie sehemu yake ya ardhi kutokana na tabia za tamaa alizokuwa ameziiga kutoka kwa viongozi wa kikoloni aliokuwa akiishi nao.

Biashara kati ya Waafrika na Wahindi pamoja na Wazungu waliobakia mjini Tanta baada ya uhuru ilikuwa ishara ya ubaguzi. Badala ya Waafrika kuwauzia Waafrika wenzao mazao ya mashamba na vitu vinginevyo vya kufanyia biashara, walienda kuwauzia Wahindi na Wazungu. Kupitia njia hii, waliziimarisha biashara za wageni hawa na hivyo basi, kuchangia pakubwa kuimarika kwa ubaguzi.

# SURA YA TATU

# SWALA LA UKOMBOZI KATIKA *MSURURU WA USALITI*

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia swala la ukombozi katika *Msururu wa Usaliti*. Tumeanzia kwa kutoa muhtasari wa riwaya hii ili tuwe na taswira kamili ya jamii husika ili itusaidie katika uchanganuzi wa kazi yenyewe. Vilevile, tumezichanganua changamoto zinazoikumba jamii ya *Msururu wa Usaliti* zikiwepo uharibifu wa mazingira, ukoloni, ufisadi, umaskini, uongozi mbaya utabaka na uozo wa jamii. Aidha, tumechanganua aina za ukombozi katika riwaya hii. Aina hizi ni ukombozi wa kimazingira, ukombozi wa kisiasa, ukombozi dhidi ya ufisadi, ukombozi dhidi ya umaskini kisha ukombozi dhidi ya uozo wa jamii.

## 3.2 Muhtasari wa *Msururu wa Usaliti*

*Msururu wa Usaliti* ni riwaya inayoiakisi hali halisi katika jamii. Katika riwaya hii, mwandishi ametumia mbinu rejeshi katika kuyaangazia matatizo yanayoikumba jamii hii. Baadhi ya matatizo haya ni uharibifu wa mazingira, ukoloni, uongozi mbaya, ufisadi, umaskini na uozo wa jamii. Uharibifu wa mazingira unaanza kujitokeza pale ambapo watu wasiojulikana wanajigawia msitu wa Rakau na sehemu za eneo zilizonyakuliwa na kufyekwa kwa maandalizi ya ujenzi. Kutokana na ufyekaji msitu huu, kisima kikubwa kilichokuwa katikati ya msitu huo kilikuwa katika hatari ya kukauka. Mwandishi pia ameuangazia ukoloni mkongwe na athari zake katika jamii ya *Msururu wa Usaliti*.

Uongozi mbaya unadhihirika kutokana na viongozi wa chama tawala ambao wanayajali maslahi yao binafsi huku wakiwa hawawajali wananchi wao. Jamii hii pia imekumbwa na ufisadi ambao unaendelezwa na viongozi wakuu serikalini kwa manufaa yao wenyewe.

Katika jamii hii pia kuna umaskini wa hali ya juu kutokana na hali kuwa serikali tawala haishughulikii matakwa ya waliotawaliwa. Hali hii inasababisha wanajamii kuumia kutokana na magonjwa wasiyoweza kuyapeleka hospitalini kwa sababu ya kukosa fedha kutokana na umaskini.

Uozo wa jamii kama vile uasherati na uzinzi, ubakaji na mauaji umejitokeza katika riwaya hii. Kutokana na madhila haya, kundi la wasomi wazalendo wanaojiita wazaliwa huru wakiongozwa na mhusika mkuu Kage, wanajiingiza katika harakati za kuikomboa jamii kutokana na madhila yanayowakumba wanajamii hawa.

Juhudi za Kage za kuyakomboa mazingira zinaendelezwa kwa bidii isiyo na kifani. Baada ya wasomi hawa kutembea kijijini, wanaiona hali halisi ya matatizo yanayowakumba wanajamii wasio na uwezo. Baada ya kukutana nao, harakati za kujikomboa kutokana na uongozi mbaya zinaanza. Hizi zinafanyika kutokana na uzinduzi wa chama kipya cha Umoja wa Wazalendo wa Taifa (UWATA), ambacho kinapigiwa debe na walio wengi kutoka upande wa upinzani. Baada ya uchaguzi kufanyika, chama hiki kinashinda na taifa jipya linazaliwa.

### 3.3 Changamoto zinazoikumba jamii ya *Msururu wa Usaliti*

Mataifa mengi barani Afrika yalikumbwa na changamoto nyingi kabla ya uhuru. Changamoto hizi zilitokana na utawala uliokuwepo wakati huo na hata wananchi wenyewe. Changamoto hizi ziliendelea hata baada ya uhuru na zinaendelea kudhihirika katika mataifa mengi yanayoendelea hadi wa leo.

Jamii ya *Msururu wa Usaliti* ilikumbwa na changamoto nyingi kabla na hata baada ya uhuru zikiwepo uharibifu wa mazingira, ukoloni, ufisadi, uongozi mbaya, umaskini, utabaka na uozo wa jamii.

#### 3.3.1 Uharibifu wa mazingira

Mazingira huharibiwa kutokana na matendo mbalimbali ya mwanadamu. Viwanda vilivyojengwa na mwanadamu huchafua hewa safi na pia taka kutoka kwenye viwanda hivyo huelekezwa kwenye chemi chemi za maji. Mnamo mwaka wa 1984, uharibifu wa mazingira ulishuhudiwa katika kiwanda cha kemikali cha Bhopal, India ambapo tani arubaini za gesi yenye sumu zilifuja na kuwaua watu elfu tatu na wengine nchini kuathiriwa vibaya kiafya. Wengi wa wale walioathiriwa waliaga dunia. Walioathirika zaidi walikuwa wanawake kupitia kupata matatizo ya kizazi, kupoteza uja uzito na hata kuzaa watoto waliokufa.

Kando na uharibifu wa mazingira kupitia viwandani, ukataji miti kiholela pia husababisha uharibifu wa mazingira. Idadi ya watu wanaofyeka misitu ili kujenga makao na majumba mbalimbali imeongezeka huku miti ya kiasili na yenye faida kwa binadamu ikiharibiwa.

Katika *Msururu wa Usaliti*, uharibifu wa mazingira umejitokeza. Uharibifu huu unaanzishwa na viongozi wakuu serikalini kulingana na habari zilizochapishwa kwenye magazeti. Kulingana na habari zenyewe, wanyakuzi hawa walikuwa wamejigawia msitu wa Rakau na shughuli za ufyekaji msitu kwa maandalizi ya ujenzi kuanza huku nayo matingatinga yakijishughulisha na ung'oaji miti. Picha kwenye gazeti hili zilionyesha shughuli hizi zikiendelea.

Wanyakuzi hawa walituhumiwa kuwa wakuu wa serikali kwa kuwa hakuna mtu wa kawaida ambaye angeweza kuwa na ujasiri wa kujikatia msitu ambao ulikuwa mali ya umma. Uharibifu huu wa mazingira kupitia ukataji miti ulikuwa na madhara makubwa kwa wakazi wa mji mkuu ambao walitegemea maji ya kisima kikubwa kilichokuwa katikati ya msitu huu. Kutokana na hili, shida ya maji ingekithiri katika eneo hili. Aidha, miti ya msitu huu ndiyo iliyosaidia kulisafishia jiji hewa iliyochafuliwa na moshi mchafu kutoka viwandani. Ukataji wa miti hii ulikuwa dhihirisho la uchafuzi zaidi wa hewa kuendelea katika jiji hili.

Uharibifu wa mazingira pia unajitokeza pale ambapo Kage analisoma gazeti la "Environist" ambapo makala hayo yalizungumzia juu ya uchafuzi wa Mto Rakau ambamo takataka kutoka kichinjio cha mji mkuu zilitupwa. Jambo hili linamfadhaisha Kage mpaka anaiandikia Halmashauri ya jiji barua ili kuijulisha juu ya uharibifu huu. Hata hivyo, Halmashauri hiyo haikuchukua hatua yoyote.

### 3.3.2 Ukoloni

Katika *Msururu wa Usaliti*, kuna aina mbili za ukoloni ambazo ni ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo.

#### 3.3.2.1 Swala la ukoloni mkongwe katika *Msururu wa Usaliti*

Katika *Msururu wa Usaliti*, tunamwona Mwamba aliyekuwa babake Mbogo akikabiliana na shida zilizosababishwa na ukoloni. Askari wa serikali ya kikoloni waliivamia nyumba ya

Mwamba kila uchao kwa madai kwamba walikuwa wakimsaka haramia Mwamba kwa sababu ya kushiriki katika vita vya kumwondoa Mzungu nchini mwao.

Jambo hili liliendelea kwa muda huku mkewe Mwamba na mwanawe Mbogo wakizidi kuhangaishwa kwa sababu ya kutoweka kwa Mwamba. Jamaa zao na hata kijiji kizima kiliingia matatani kwa sababu ya Mwamba mpaka wote wakaanza kumlaumu. Licha ya haya yote, mkewe Mwamba hakumsaliti mumewe kamwe katika mateso aliyoyapitia. Haya yanadhihirishwa na maneno yafuatayo:

> Mamake Mbogo tu ndiye aliyesimama tisti kuumuunga mkono mumewe. Alifanya hivi kwa kuamini kuwa mumewe aliingia vitani kwa sababu ya uzalendo na kudai kuwa wale waliomlaumu walikuwa waoga walioogopa kupigana na wakoloni kulikomboa taifa lao (uk. 50).

Kilele cha vita kilikuwa kuchomwa kwa kambi ya askari wa serikali ya kikoloni. Baada ya tukio hili, Mwamba alirudi nyumbani usiku huku akijificha. Baada ya kula alichukua bunduki yake na kutoweka. Asubuhi, kijiji chote kilikuwa kimezingirwa na askari wa kikoloni huku wakifanya msako nyumba hadi nyingine. Tukio hili ndilo lililosababisha kukamatwa kwa wanaume wengi katika kijiji hiki. Ajabu ni kuwa mkewe Mbogo ndiye aliyekuwa mwanamke wa pekee kukamatwa. Walipopelekwa kifungoni hawakurudi tena. Mkewe Mwamba alipatana na hali ngumu na kutwaliwa na mauti akiwa huko.

> Mamake Mbogo hakurudi kutoka kifungoni. Kutokana na kipigo alichopata wakati alipokuwa akikamatwa na mateso baadaye, aliishia kuwa mgonjwa.Waliomzuilia waliuachia ugonjwa ukamtafuna mpaka ukammaliza. Hata maiti yake haikuonekana. Ilitupwa kama mzoga wa mbwa katika kaburi la pamoja walimotupwa wafungwa waliofia kizuizini… (uk.53).

Hili lilikuwa pigo kubwa sana kwa Mbogo aliyekuwa mwanawe Mwamba na aliyeachwa kujitunza na kujikimu maishani akiwa na umri mdogo sana. Baadaye, uhuru ulipatikana huku wanajamii wakiwa na matumaini makubwa ya kuona mabadiliko kutokana na uongozi mpya wa Waafrika wenzao. Muda ulivyozidi kupita, wanajamii hawakuyaona mabadiliko waliyokuwa wakiyatarajia. Badala yake, ukoloni mamboleo ulienea katika jamii hii.

#### 3.3.2.2 Swala la ukoloni mamboleo katika *Msururu wa Usaliti*

Katika *Msururu wa Usaliti*, ukoloni mamboleo ulianza punde tu baada ya uhuru. Kwanza kabisa, masetla walioishi nchini hawakuondoka na badala yake walihakikishiwa ulinzi kamili. Waafrika nao kwa upande mwingine walikereka zaidi kutokana na ahadi za uongo walizowekewa na utawala mpya wa Mwafrika. Kwa mfano, wapiganiaji uhuru waliosalia msituni waliagizwa watoke na kujiunga na wananchi wenzao katika ujenzi wa taifa, huku wakihaidiwa msaada wa kuwawezesha kuanzia maisha upya. Punde tu baada ya kurudi vijijini, serikali mpya iliwasahau kabisa. Mwamba alikuwa mmoja wa waliowekewa ahadi hizi za uongo baada ya kupoteza kila kitu akipigania uhuru. Haya yanadhihirishwa na maneno yafuatayo:

> … Alirudi kijijini akiwa mzee aliyepoteza kila kitu akilipigania taifa lake, alipoteza ujana wake, afya, shamba na familia. Hakufidiwa kwa njia yoyote, wala mchango wake kutambuliwa. Alikufa kwa umaskini na kutelekezwa… (uk. 54).

Kwa upande mwingine, msitu wa Rakau ulinyakuliwa na viongozi wakuu serikalini. Hawa walikuwa viongozi waliochukua hatamu baada ya taifa kujinyakulia uhuru. Ufyekaji miti ulianza ili waanze kujenga majumba makubwa. Huu ulikuwa ukoloni mamboleo wa kuwakandamiza wananchi kwa kuwa unyakuzi huu haukuwafaidi wao, bali uliwafaidi viongozi hawa. Majumba waliyonuia kuyajenga hayakuwa kwa manufaa ya wananchi, bali kwa manufaa ya wanyakuzi wenyewe.

Jambo hili linaafikiana na mawazo ya Karl Marx katika nadharia yake ya U-Marx katika Wamitila (2006: 182-184) kuwa historia ya maisha ya binadamu ni harakati za kitabaka. Hatua ya juu ya mwendeleo wa utabaka ni uzukaji wa mfumo wa ubepari ambapo mali humilikiwa na watu wachache. Hili linaonyeshwa katika uyakinifu wake kwa kuwa unyakuzi wa ardhi uliwafaidi wachache tu walioushiriki mfumo wa ubepari na ambao ni viongozi wa serikali.

Kuachishwa kazi kwa Daktari Makau kulikuwa sehemu ya ukoloni mamboleo. Daktari huyu aliandikiwa barua ya kuachishwa kazi kama daktari katika hospitali kuu ya Ngomekati na Alade, aliyekuwa katibu mkuu wa kudumu. Kulingana na barua hii, Daktari Makau aliachishwa kazi kwa madai kuwa alitumia muda wake mwingi katika shughuli za kisiasa, hasa kufanyia kampeni

upande wa upinzani. Aidha, alisemekana kuwa alivunja sheria iliyowakataza wafanyikazi wa umma kushiriki katika siasa.

Jambo hili lilimkera sana Daktari huyu ambaye alikuwa kielelezo cha jamii kwa kufanya kazi katika mazingira duni bila hata kufikiria kuanzisha kliniki yake binafsi kama wenzake walivyokuwa wakifanya baada ya kulipwa mishahara duni. Uzalendo wake ulilipwa kwa uovu na dhuluma. Daktari Makau alizidi kushangaa kwa kuwa hakukuwa na sheria yoyote iliyomkataza mtumishi wa umma kujiunga na chama cha kisiasa. Ukweli ni kuwa Daktari huyu alidhulumiwa kwa kuwa aliunga mkono upinzani badala ya kuunga mkono chama tawala ambacho kilidhaniwa kuwa chama pekee kilichofaa kuitawala nchi siku zote. Haya yanaungwa mkono na maneno yafuatayo: "Daktari Makau alidhulumiwa kwa kufurahia uhuru wake wa kuunga mkono upinzani. Kwa kufanya hivi, alichukuliwa kuwa adui wa dola" (uk. 110).

Kwa upande mwingine, kuacha kazi kwa Kanali Upepo kulikuwa zao la ukoloni mamboleo. Kanali upepo alikuwa mwanajeshi aliyekuwa bora kiasi cha kupandishwa cheo hadi akawa kapteni. Kutokana na ufanisi wake, alipelekwa India kwenda kusomea uhandisi wa vyombo vya kijeshi kama vile meli za kubebesha silaha, meli za mapambano na nyambizi na utunzaji na urekebishaji wa mitambo ya vyombo hivyo. Baada ya mafunzo haya, Kapteni Upepo alihisi kuwa alifaa kupata mafunzo ya uundaji wa vyombo hivi. Wataalamu wake walikataa kwa kumwarifu kuwa hiyo haikuwa sehemu ya mkataba wa mafunzo baina yao na nchi yake. Kapteni Upepo alielewa kuwa hakukatazwa mafunzo haya kwa sababu halali, bali kwa sababu ya utegemezi uliowakilisha ukoloni mamboleo.

Alielewa itikadi iliyotawala nchini mwake ilikuwa utegemezi wa kudumu. Kwa hivyo, wataalamu wake hawakuhitaji kufunzwa kuwa wavumbuzi na watengenezaji wa vitu vya Marekani. Badala yake walifunzwa kuwa warekebishaji wa vyombo vilivyoagizwa kutoka Amerika, Ulaya, Uchina na hata India. Kazi yao ilikuwa kama mafundi (uk. 124).

Kulingana na akili na uwezo wake, Kapteni Upepo alionelea kuwa ilikuwa lazima afanye juu chini ajifunze jinsi ya kutengeneza meli. Alifanya utafiti kwenye vitabu mbalimbali na hata kwenye tovuti mbalimbali katika mitandao. Baada ya mwaka mmoja wa utafiti, aliitengeneza

meli yake na kuifanyia majaribio. Kutokana na ufanisi wake, Kanali Upepo alipata barua ya uhamisho kwa madai kuwa alikuwa amepandishwa cheo. Lengo hasa halikuwa kumpandisha cheo, bali kumwondoa ili afisa aliyependelewa kazini apewe kazi ya ukurugenzi utendaji katika kampuni hiyo. Kutokana na kutoridhika kwake kuhusiana na kitendo hiki, Kanali Upepo aliamua kuiacha kazi na kwenda kuianzisha kampuni yake. Hili ni jambo ambalo halikustahili kufanyiwa mtu mwenye ujuzi wa hali ya juu kama huyu. Badala yake wangemwacha autumie ujuzi na tajriba aliyokuwa nayo kuiendeleza na kuiimarisha kampuni.

### 3.3.3 Ufisadi

Neno ufisadi kwa kawaida lina maana ya maovu au uharibifu wa aina yoyote ile. Aidha, ufisadi ni matumizi ya madaraka au mamlaka katika ofisi za umma au za kibinafsi kwa manufaa ya mtu binafsi au kundi la watu. Ufisadi unaweza kuwa wa kiwango cha chini au wa kimataifa. Ufisadi wa kiwango cha chini ni sakata zinazohusisha watu wa kawaida kila siku katika jamii. Mifano ya aina hii ya ufisadi ni upokeaji wa rushwa kwa maafisa wa trafiki kutoka kwa wenye magari yenye kasoro barabarani ili wasiadhibiwe kulingana na sheria, kutoa kitu kidogo ili faili zipatikane ofisini na mengineyo. Ufisadi wa kiwango cha kimataifa nao huhusisha utoaji na upokeaji wa mabilioni ya pesa.

Ufisadi katika nchi nyingi za Afrika huimarishwa na tamaa inayowasukuma watu kunyakua vitu vya umma au vya wengine kiharamu. Aidha, sheria dhaifu za nchi nyingi za Afrika huchangia pakubwa kwa kuwa mafisadi hufahamu kuwa serikali hizi hazitawachukulia hatua. Usimamizi mbaya wa fedha na mali ya umma pia huchangia ufisadi. Ufisadi huu una madhara mengi. Haya ni kama vile kupotea kwa pesa nyingi za umma, kukithiri kwa umaskini katika nchi, kuhama kwa wawekezaji na kwenda kuwekeza kwenye nchi zisizo fisadi na uchumi wa nchi kuzorota na wananchi kuishi katika dhiki na taabu isiyokadirika. Kwa mujibu wa mihimili ya Nadharia ya U-Marx katika Wamitila (2006), “historia ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo itachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi na pia huathiri uzalishaji mali na usambazaji mali hizo” (uk. 182).

Katika *Msururu wa Usaliti*, baadhi ya wahusika wamejinyakulia mali kwa njia zisizofaa. Huu ni mojawapo wa aina za ufisadi. Kipanga, aliyekuwa askari wa jela na mwenye cheti cha kidato cha

nne tu, anapaa kimiujiza na kufikia kiwango cha kuwa bilionea. Katika kupaa kwake, anasaidiwa na mjomba wake aliyekuwa na uhusiano mzuri na mbunge wao ambaye alikuwa waziri katika serikali. Aidha, mbunge huyu alikuwa na uhusiano mzuri na kiongozi wa nchi. Kipanga na mjomba wake wanapanga safari ya kwenda kumwona waziri ili amsaidie kupata kazi. Baada ya kufika kwenye ofisi ya waziri na kufanya mazungumzo mafupi, Kipanga anapewa zabuni ya kutoa ugavi wa tarakilishi katika wizara mbalimbali papo hapo. Biashara hii inampatia Kipanga utajiri mkubwa.

> Biashara ya Kipanga ilivyoleta pesa kwa wingi kama mchanga wa bahari, miaka miwili ilimtosha kuzaliwa upya. Kutoka askari wa jela aliyepewa shilingi elfu tano kwa mwezi, sasa alikuwa milionea aliyeweza kuwaajiri askari elfu moja. Hivi ndivyo mamilionea wa Kiafrika walivyozaliwa (u.k 46).

Hali ya kuwa na pesa nyingi ilimletea Kipanga wazo la kuwekeza. Baada ya kufikiria kwa muda jinsi ya kupata ardhi ya kufanyia uwekezaji, alionelea ni heri arudi kwa yule waziri aliyemsaidia kupata kazi. Hapa waliendeleza ufisadi zaidi na kipanga akapewa kipande cha ardhi cha Halmashauri ya jiji, kilichokuwa kimetengwa kwa ujenzi wa hospitali ya umma. Waziri alimtengenezea Kipanga karatasi za kuonyesha umilikaji wa ardhi hiyo. Bila kukawia, Kipanga alijenga gereji iliyokuwa na sehemu ya kuuzia mafuta, duka la vipuri na karakana ya kurekebisha magari. Huu ni ufisadi wa hali ya juu.

Aidha, Mbogo, ambaye ni mmoja wa wahusika wakuu katika *Msururu wa Usaliti* anaendeleza ufisadi kwa kuwanunua wabunge na madiwani walioshinda katika vyama vya upinzani ili warudi kwenye chama tawala. Alishirikiana na Mzee (rais wa nchi) katika kutekeleza jambo hili.
Shughuli ya kuwanunua wabunge na madiwani hawa iligharimu mamilioni ya pesa kwa kuwa baada ya kununuliwa, uchaguzi ulifanywa tena kwa maana kuwa kiti kiliachwa wazi baada ya uhamaji. Chama tawala kiligharamia shughuli yote ya kampeni na uchaguzi na baada ya ushindi, sherehe kubwa ilifanywa kwenye ikulu ili kuwakaribisha nyumbani washindi hawa.

Kifo cha Makena kilitokana na ufisadi uliopangwa na mumewe Mbogo. Baada ya Mbogo kugombana na mkewe na kuachana kwa muda, alisikia tuhuma kwamba mkewe alitaka kugombea kiti cha ubunge cha Rware. Jambo hili lilimtia wasiwasi na hofu Mbogo aliyekuwa

mbunge wa Rware wakati huo kwa kuwa alifahamu vizuri kuwa mkewe alikuwa na uhusiano mzuri sana na wanakijiji na wangeweza kumchagua kama mbunge kwa urahisi sana. Kutokana na haya, alimwendea Mdudu aliyekuwa mfanyikazi wake na pamoja wakampangia mauti kupitia kwa ajali.

> Alimweleza mwajiri wake hivi: *Toyota Corolla* ya Makena itakuwa inateremka kwenye barabara hii ikiwa nyuma ya kifaru. Katikati ya mteremko kigari hiki kitakuwa kinabingirika kama jiwe kutoka milimani. Kumbuka nitakuwa nimeharibu breki zake kwa siri. Ghafla, nitafunga breki katikati ya barabara. Toyota Corolla itagonga kifaru kwa nyuma na kusagwasagwa… Dereva wa kigari hiki akipona, njoo uchukue pesa zako (uk. 211).

Baada ya Mbogo na Mdudu kuikamilisha mipango yao, utekelezaji ulifanywa na kisha Makena akaaga dunia kwa njia ya kikatili.

### 3.3.4. Umaskini

Umaskini ni hali ya kutokidhi mahitaji mbalimbali ya kila siku kwa kiwango kinachofaa. Hali hii husababishwa na walio wachache katika jamii kuhodhi nyenzo zote za uzalishaji mali huku walio wengi wakiachwa bila chochote ila tu nguvu zao ambazo wanaziuza kwa wale wanazozihitaji ili wapate ujira mdogo wa kuyaendeleza maisha yao. Maelezo haya yanaunga mkono sehemu ya nadharia ya U-Marx inayosema kuwa umaskini ni zao la utabaka. Umaskini ni swala la kiuchumi ambalo hupaliliwa na mfumo wa siasa uliopo na unaolenga kunufaisha wachache. Kwa mujibu wa mihimili ya nadharia ya U-Marx katika Wamitilla (2006:182-184), historia ya maisha ya binadamu ni harakati za kitabaka ambapo hatua ya juu ya mwendeleo wa utabaka ni uzukaji wa mfumo wa ubepari ambapo mali humilikiwa na watu wachache. Mali hii hutokana na juhudi za watawala za kuwakandamiza watawaliwa; hasa wafanyikazi.

Baada ya uhuru, Mwamba, aliyekuwa babake Mbogo alirudi kutoka msituni na kuishi katika hali ya umaskini mwingi. Hii ilitokana na hali kuwa ardhi yake ilitwaliwa na wakoloni alipokuwa msituni akipigania uhuru. Aidha, aliporudi nyumbani, afya yake ilikuwa imedhoofika kiasi cha kutoweza kufanya kazi ili kujipatia mali yoyote. Aliishi katika hali ya umaskini hadi kifo chake. Baada ya kifo cha Mwamba, Mbogo aliachwa yatima kwa kuwa mamake alikuwa amekufa akiwa kizuizini. Katika uyatima wake, aliishi kuendeleza hali ya umaskini aliyoachiwa na

babake baada ya kifo chake. Ilimbidi ajitegemee na kukabiliana na uhalisia wa maisha huku akiwa hana rasilimali yoyote aliyoirithi kutoka kwa wazazi wake. Hali hii ilimfanya atafute vibarua kwenye mashamba ya watu ili apate pesa za kununua chakula. Baada ya muda, alihamia Uleleni na kuajiriwa na mmoja wa masetla ambao hawakuondoka baada ya uhuru kwa jina Bwana Mark ili aendelee kujikimu maishani.

Umaskini pia unadhihirika katika mji wa Rware ambapo wagonjwa waliokuwa wamepimwa na kupatikana na UKIMWI hawakuweza kumudu kujinunulia dawa. Aidha, magonjwa yenye tiba kama vile malaria yaliua watu kwa sababu umaskini uliwafanya washindwe kununua dawa. Sera ya kugawana gharama ya matibabu kati ya wananchi na serikali haikuwa rahisi kwa sababu ya umaskini. "Kuwataka kugharamia dawa ilikuwa ni kama kumwambia mtu anayeteketezwa na moto achote maji ya kuuzima ili ajiokoe" (uk. 138).
Maelezo haya ni ithibati tosha kuwa wakazi wa mji huu walikuwa wakiishi katika hali ya umaskini uliokuwa umekithiri.

### 3.3.5 Uozo wa jamii

Uozo wa jamii ni hali ambapo maovu mengi na yasiyotarajiwa hutendeka katika jamii. Maovu haya yanaweza kutendwa na wananchi kwa wananchi wenzao na pia viongozi kwa wananchi wao. Uozo wa jamii unaweza kujitokeza katika hali tofauti tofauti. Katika kazi husika, uozo wa jamii umejitokeza katika hali za mauaji, ubakaji, uasherati na uzinzi.

#### 3.3.5.1 Mauaji

Mauaji ni hali ya kutoa uhai wa binadamu au hata mnyama kwa kukusudia au hata bila kukusudia. Katika jamii ya *Msururu wa Usaliti*, mauaji yanayotekelezwa ni ya kukusudia. Mhusika mkuu Mbogo anashiriki katika vitendo kadhaa vya uuaji. Kwanza, anamuua Igweta aliyekuwa amezeeka na afya yake kudhoofika sana. Mauaji haya yanatokana na tamaa yake ya utajiri baada ya ndoto yake ya maisha kutimia na kuanza kupanda daraja la utajiri. Baada ya kuuziwa kipande cha kwanza cha ardhi yenye mibuni na Igweta, Mbogo anagundua kuwa kilimo cha mibuni kingeweza kumletea utajiri mkubwa. Kwa sababu hii, anarudi kwa mzee Igweta na kumsihi amwuzie kipande kingine cha ardhi. Igweta hakubali kumuuzia kipande kingine. Jambo hili linamghadhabisha sana Mbogo na kuanza kumchukia Igweta. Usiku wa manane, anakwenda

kwenye nyumba ya Igweta na kuifinya shingo yake dhaifu. Igweta anakata roho na kisha Mbogo anafuta alama zote za uuaji na kurudi kwake.

Habari za kifo cha Igweta haziwashtui wanakijiji kwa kuwa walikuwa hawamtembelei kwa tuhuma kuwa alikuwa mchawi. Mtu wa pekee aliyemtembelea alikuwa Mbogo na ndiye mwanakijiji wa pekee aliyejishughulisha na mazishi ya Igweta akisaidiwa na askari. Baadaye, Mbogo analima sehemu ya ardhi iliyokuwa imebakia na kupanda mibuni.

Aidha, Mbogo alishiriki katika mauaji ya bibi yake. Wakati huu, yeye ndiye aliyekuwa Mbunge wa Rware. Baada ya kukosana na mkewe, alisikia minong'ono kuwa alikuwa akitaka kuwania kiti cha ubunge cha Rware. Jambo hili halikumfurahisha Mbogo. Baada ya mwezi mmoja, Mbogo alikwenda kumshawishi bibi yake warudiane. Kwa sababu ya utu wa Makena aliyekuwa bibi yake Mbogo, alisahau tofauti zake na Mbogo na kurudi kwake. Jambo ambalo hakulifahamu Makena ni kuwa kurudi kwake kulikuwa njama ya kumwua ili asiweze kumshinda katika uchaguzi wa ubunge wa Rware. Mbogo pamoja na Mdudu aliyekuwa mfanyikazi wake walipanga njama yote na mambo yakaenda kama yalivyopangwa hadi Makena akapoteza maisha yake.

Habari za kifo cha Makena zilimfikia Kage aliyekuwa binti yake kwa mshangao mkuu akiwa masomoni Uingereza. Kage hakuridhishwa na kifo cha mamake na alikuwa na hisia kali kuwa mamake alikuwa ameuliwa; jambo ambalo alikuja kuthibitisha baadaye kuwa la ukweli.

> Maswali mengi yalizuka katika akili ya Kage, hasa alipoelezwa kwamba ajali ilitokea mchana. Kwa nini gari la mamake liligongana na lori? Nani hasa alilaumika katika ajali, na ni hatua gani zilichukuliwa?... Alinuia kutafuta majibu ya maswali haya pindi akimaliza masomo na kurudi nyumbani. (uk. 25).

Maneno haya yanadhihirisha kuwa Kage aliendelea kuwaza sana juu ya kifo cha mama yake hata baada ya mazishi hadi pale alipokuja kubaini ukweli wa tukio lenyewe.

#### 3.3.5.2 Ubakaji

Ubakaji ni uovu uliokithiri katika nchi nyingi barani Afrika na hata ulimwengu mzima. Matukio ya ubakaji yameendelea kushika kasi katika nchi mbalimbali duniani licha ya kuwepo kwa sheria za kuwabana wahusika. Utafiti uliofanywa na UNICEF kati ya mwaka 2000 hadi 2011 ulionyesha kuwa Afrika ya Kusini ndiyo nchi yenye idadi kubwa ya kesi za ubakaji duniani wanazofanyiwa watoto wadogo. Mwaka wa 2009 jumla ya kesi 67,000 ziliripotiwa. Nchi ya Botswana inashikilia nafasi ya pili kwa matukio ya ubakaji.

Katika mwaka wa 2011, wanawake zaidi ya 600 walifanyiwa vitendo vya ubakaji. Nchi ya Lesotho nayo ndiyo inayochukua nafasi ya tatu katika ubakaji huku asilimia 33 ya wanawake waliobakwa wakiwa na umri wa miaka 18 na pia kukiwa na asilimia 66 ya kesi za ubakaji kila mwaka.

Jamii ya *Msururu wa Usaliti* imekumbwa na uovu wa ubakaji. Uovu huu unatekelezwa na mhusika Mbogo akiwa mbunge wa Rware. Mbogo alimbaka mhudumu wake wa nyumbani. Baada ya tendo hili msichana huyu alikimbilia kwao na Mbogo kumficha mkewe ukweli wa mambo. Makena aliwaza kuwa kulikuwa na sababu kisha akafululiza hadi kwa wazazi wa msichana ili aweze kufanya uchunguzi. Baada ya ukweli kuwekwa wazi, Makena aligombana na mumewe Mbogo; jambo ambalo lilimfanya Makena kuondoka na kwenda kukodisha nyumba. Aliendeleza kesi ya ubakaji hadi ithibati ikapatikana kisha Mbogo akakamatwa na kuwekwa seli.

#### 3.3.5.3 Uasherati na uzinzi

Uasherati ni hali ya kufanya tendo la ndoa kabla ya ndoa. Uzinzi nao ni hali ya kufanya tendo la ndoa nje ya ndoa. Kwa hivyo, mtu ambaye hajaoa wala kuolewa anapojamiana na mtu mwingine huwa anafanya uasherati. Naye mtu aliye ndani ya ndoa anapojamiana na mtu mwingine mbali na mkewe au mumewe huwa anafanya uzinzi. Katika nchi nyingi ulimwenguni, maovu haya yamekithiri na ndiyo njia inayoongoza katika kueneza virusi vya UKIMWI. Utafiti uliofanywa na shirika la “ United Nations Children’s Education Fund” (UNICEF), kati ya mwaka wa 2000 na mwaka wa 2011 ulionyesha kuwa katika nchi ya Swaziland, kesi za uambukizaji wa virusi vya UKIMWI kwa wasichana wa miaka 18 umekuwa ukiongezeka. Ripoti hii ilionyesha kuwa msichana mmoja kati ya watatu huwa na virusi vya UKIMWI.

Katika *Msururu wa Usaliti*, uasherati unadhihirika kupitia kwa mhusika Agutu ambaye alikuwa mpenzi wake Daktari Makau na ambaye walikuwa wamepanga kuoana. Kutokana na urembo wa Agutu na tamaa ya pesa, maisha yake yalibadilika na kuanza kufanya uasherati na wateja wake waliokuwa na akaunti zenye pesa nyingi.

> Akaunti za wateja waliomvutia zaidi Agutu ziliingia pesa chururu! Kama maji yatiririkavyo mtoni kwa kasi. Hawa ni watu ambao walitembelea benki na kuongeza akiba zao kuliko walivyoingia kutoa. Mamilionea waliofanya biashara zilizotembea kwa miguu ya siasa (uk. 149).

Kupata hata elfu hamsini kwa Agutu kutokana na biashara ya uasherati na uzinzi hakukuwa shida. Kwa mara ya kwanza, alianza na Owawa aliyekuwa mkurugenzi wa kampuni ya ujenzi wa barabara na aliyekuwa mkwasi mkubwa. Baada ya muda, mkewe Owawa alikuja kugundua uovu wa mumewe na kuwafumania katika hoteli moja huku wakiendeleza starehe zao. Bibi yake Owawa alizusha vurumai na kwa bahati nzuri, Agutu aliponyoka na kutoweka huku Owawa akibakia kupigwa vibaya na mkewe. Huu ndio uliokuwa mwisho wa uhusiano kati ya Agutu na Owawa.

Hamu ya pesa kutokana na biashara hii ilimwandama Agutu na kumwelekeza kwa Mbogo na hatimaye Kipanga. Alijipatia pesa nyingi zilizomwezesha kubakia bila deni yoyote. Wakati wa kuoana ulipofika, Daktari Makau alihamia katika nyumba kubwa na kumwalika Agutu wakae huko huku wakifanya mipango ya arusi. Agutu hakupendezwa na wazo hili na kwa hivyo alisita kuhamia kwa Daktari Makau. Mpenzi wake Agutu alikuwa na hamu ya kuoa ila tu hakujua kuwa sababu ya Agutu ya kukawia kuhamia kwake ilikuwa ni kunaswa katika mtego wa uasherati na uzinzi.

Kutokana na tabia za Agutu, aliambukizwa virusi vya UKIMWI na baadaye kuaga dunia. Wakati huu, Owawa alikuwa amekufa mwaka mmoja uliopita. Mbogo naye alikuwa ameambukizwa virusi vya UKIMWI na afya yake kuanza kudhoofika. Kwa bahati nzuri, Daktari Makau hakuwa ameambukizwa virusi hivi. Alidhihirisha haya baada ya kwenda kupimwa akiwa na mpenzi wake Nafula.

Mbogo naye anadhihirisha uzinzi kwa kufanya mapenzi na wanawake wengine nje ya ndoa. Alianza haya baada ya kutajirika na kuingia katika siasa. Jinsi alivyopata utajiri mwingi kutokana na siasa ndivyo alivyoendelea kuwa mzinzi. Haya yanadhihirishwa na maneno yafuatayo: "Mbogo alizidi kutajirika, halafu akaingia katika siasa. Pesa na madaraka ya kisiasa yakazua ulevi mkubwa wa wanawake" (uk. 206).

Uzinzi wa Mbogo uliendelea huku mkewe akivumilia na kutotaka kuzua vurugu kwa kuogopa ndoa yao kuvunjika. Tabia hii ilifikia kilele pale ambapo alimbaka mfanyikazi wao wa nyumbani. Jambo hili lilimfanya awekwe seli kwa muda wa siku tatu na kutozwa faini ya shilingi elfu mia tano kwa uovu alioufanya.

### 3.3.6 Utabaka

Utabaka ni mfumo wa kijamii unaowagawa watu kwenye makundi kutegemea uwezo wao wa kiuchumi au kijamii. Karl Marx katika Wamitila (2006) anasema, "historia ya maisha ya binadamu ni harakati za kitabaka. Hatua ya juu ya mwendeleo wa utabaka ni uzukaji wa mfumo wa ubepari ambapo mali humilikiwa na wachache" (uk. 182). Sarara (1997) akimnukuu Ngara (1985), anasema kuwa katika jamii yenye matabaka, nguvu za kiuchumi huwa na watawala ambao huhodhi nyenzo za uzalishaji mali. Anaendelea kusema kuwa tabaka hili la juu ndilo pia husimamia elimu na itikadi katika jamii. Mawazo, imani na itikadi ya tabaka tawala huchukuliwa kuwa ya jamii nzima.

Katika *Msururu wa Usaliti*, kuna matabaka ya waliosoma na wasiosoma, viongozi na watawaliwa, matajiri na maskini. Tabaka la waliosoma linawakilishwa na vijana wasomi ambao wanajiita "Wazaliwahuru". Tabaka hili linajumulisha akina Kage, Daktari Makau, Agutu, Nafula na Kanali Upepo. Tabaka hili ndilo linalochukua nafasi kubwa ukombozi wa jamii unapoanza. Wasiosoma nao ni wananchi wa kawaida ambao hawakupata nafasi ya kujiungana na shule. Hawa ni kama vile wanakijiji wa Itungi alikozaliwa Kage wakiwemo Naito na Magu ambao walikuwa wazazi wa Sarah ambaye alikuwa mfanyikazi wa Kage.

Tabaka la viongozi nalo lilijumuisha kiongozi wa nchi (Mzee), wabunge kama vile Mbogo, mawaziri na madiwani. Watawaliwa nao walikuwa wananchi wa kawaida waliokuwa chini ya

uongozi wa viongozi hawa. Matabaka ya juu na ya chini yanadhihirika pale ambapo Kage anaenda shuleni akiwa amevalia viatu huku wanafunzi wenzake wakitembea miguu mitupu. Kage anawakilisha tabaka la juu huku wanafunzi wenzake wakiwakilisha tabaka la chini.

Mgawanyiko wa kitabaka unadhihirishwa na uwekezaji wa biashara unaogharimu pesa nyingi kama vile hoteli ya Mlima Tembo ambayo wamiliki wake aghalabu ni watu wa tabaka la juu. Vilevile wateja wake ni watu wa tabaka la juu kama vile Kipanga. Kwa upande mwingine wanyonge hawawezi kumudu bei za hoteli kama hizi na wanalazimika kutafuta hoteli duni ambazo bei zake wanaweza kukabiliana nazo.

### 3.3.7 Uongozi mbaya

Uongozi mbaya ni changamoto inayozikumba nchi nyingi barani Afrika. Kutokana na uongozi wa aina hii, wananchi wanakandamizwa na kunyimwa haki zao. Uongozi mbaya pia unahusisha ubadilishaji wa katiba ili iweze kuwafaa viongozi walio mamlakani na waweze kuongoza nchi kwa muda mrefu. Hili ni jambo ambalo limeshuhudiwa katika baadhi ya nchi barani Afrika. Kutokana na kufinyiliwa kwa wananchi na uongozi huu, viongozi wa upinzani wameanza kufanya majaribio ya mapinduzi ili wananchi waweze kupata haki, jambo ambalo serikali tawala zinaendelea kutupilia mbali.

Jamii ya *Msururu wa Usaliti* imetawaliwa na uongozi mbaya. Viongozi waliolinyakulia taifa uhuru wanataka kuendelea kuitawala nchi kwa mabavu kupitia kwa chama kimoja tu cha utawala kilichoundwa baada ya uhuru. Viongozi wa serikali kama vile Mzee na Mbogo aliyekuwa mbunge wa Rware wanaamini kuwa wananchi hawafai kujiunga na vyama vya upinzani. Wanaojiunga na vyama hivi wanachukuliwa kuwa wasaliti wa serikali tawala. Kutokana na uongozi wa aina hii, Daktari Makau anaachishwa kazi kwa kuunga mkono upinzani. Uongozi mbaya pia unamfanya Kanali Upepo kuacha kazi baada ya kudaiwa kupandishwa cheo; jambo ambalo lilinuiwa kumnufaisha mtu mwingine bali si yeye.

Diwani Kirera naye anafunga barabara ya umma iliyowawezesha wananchi kufikia barabara kuu ya lami kwa madai kuwa njia yenyewe ilipitia shambani mwake na kwa hivyo alitaka kuifanya sehemu ya mali yake. Ukweli ni kuwa hii ndiyo iliyokuwa njia rasmi katika ramani ya

mashamba iliyohifadhiwa katika ofisi ya ardhi. Sababu kuu ya kufanya hivi ni kuwa alikuwa diwani wa chama tawala baada ya kuuhama upinzani na zaidi alikuwa na uhusiano wa karibu na mheshimiwa Mbogo. Kutokana na haya, alijiona huru kutenda jambo lolote aliloliona likimfaa mwenyewe hata kama lilikuwa likiwakandamiza wananchi. Hata ripoti kumuhusu ilipopelekwa kwa chifu, hakumchukulia hatua yoyote kwa kuwa alimwogopa kwa uhusiano wake na mheshimiwa Mbogo na pia kwa kuwa alikuwa kibaraka wa chama tawala.

Magu kwa upande mwingine anakifanyia kazi chama tawala kwa muda mrefu na hatimaye analipwa kwa dhuluma. Magu alikuwa mkuu wa tawi la vijana la chama tawala. Kutokana na cheo chake, alipata umaarufu mkubwa. Usaliti wa kisiasa ulimwondoa mamlakani kwa madai kuwa alikuwa amemhasi rais, aliyekuwa kiongozi wa chama tawala. Wakati huohuo alishikwa na kuwekwa kizuizini kwa muda wa miaka kumi. Humo kizuizini alifanyiwa ukatili uliokithiri kwa kutolewa uume wake. Baada ya kumaliza kifungo chake, Magu alirudi kijijini akiwa mwananchi wa kawaida na kuipata familia yake katika hali mbaya ya umaskini. Kuanzia wakati huo, maisha yake yalibadilika na kuwa ya ulevi mtupu.

Kutokana na changamoto wanazozipitia wanajamii hawa, wanabaki bila lingine la kufanya ila tu kujiingiza katika juhudi za kujikomboa kutokana na baadhi ya changamoto hizo.

### 3.4. Ukombozi katika *Msururu wa Usaliti*

Kwa mujibu wa nadharia ya U-Marx katika Wamitila (2006) “ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali kutokana na juhudi za wafanyikazi au wenyewe utaishia kujiangamiza kutokana na mbegu za maangamizi unazozisheheni” (uk. 182). Marx anaendelea kusema kuwa njia ya kusaidia na labda kuharakisha kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushtumu na kufichua batili iliyopo katika itikadi za kibwanyenye inayoimarisha ubepari.

Kulingana na maelezo haya, viongozi wa jamii ya *Msururu wa Usaliti* waliuendeleza mfumo wa ubepari na ndio chanzo cha changamoto tulizozielezea zikiwepo uharibifu wa mazingira, ukoloni, ufisadi, uozo wa jamii, umaskini, utabaka na uongozi mbaya.

Wanajamii waliokandamizwa kwa muda mrefu kupitia kwa mfumo wa ubepari wanajiingiza katika harakati za kushtumu na hata kufichua uovu uliokuwa katika itikadi za viongozi mabwanyenye na ambazo ziliimarisha ubepari. Harakati hizi zinaongozwa na vijana wasomi ambao walikuwa wazalendo waliojiita wazaliwahuru. Kufuatia nadharia hii ya U-marx, wazalendo hawa wanajiingiza katika harakati za kuikomboa jamii bila kungojea mfumo wa ubepari ujiangamize wenyewe.

### 3.4.1 Aina za ukombozi katika *Msururu wa Usaliti*

Kabla ya uhuru, nchi za bara la Afrika hazikushiriki katika kujikomboa kwa awamu moja. Ukombozi ulifanywa kwa viwango mbalimbali kulingana na shida tofauti zilizowakabili wananchi kwa wakati huo. Hata baada ya uhuru wa bendera kwa mataifa mengi barani hili, shida nyingi zinaendelea kuwakabili wananchi. Kujikomboa kutokana na shida hizi hakufanyiki kwa wakati moja bali kufuatia viwango mbalimbali kutegemea aina na uzito wa matatizo haya.
Vile vile, wanajamii wa *Msururu wa Usaliti* hawaanzi kujikomboa kutokana na shida zinazowakabili kwa wakati mmoja, bali kwa viwango kwa kuwa ukombozi wenyewe ni wa aina tofauti tofauti.

#### 3.4.1.1 Ukombozi wa kimazingira

Ukombozi wa kimazingira ni hali ya kulinda mazingira asilia kwa misingi ya kibinafsi, kupitia kwa mashirika na hata kuhusisha serikali kwa manufaa ya mazingira asilia yenyewe na hata binadamu. Kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu duniani na viwango vya juu vya teknolojia, mazingira yanaendelea kuharibiwa. Jambo hili linachukuliwa kwa uzito na serikali za nchi mbalimbali zimeanza kukomesha shughuli zinazosababisha uharibifu wa mazingira.

Katika *Msururu wa Usaliti*, mwandishi amekazia swala la kuyakomboa mazingira kupitia kwa Kage ambaye ni mmoja wa wahusika wakuu. Kage ni mwanamke msomi na mzalendo ambaye anashirikiana na vijana wenzake katika juhudi hizi muhimu.

Waandishi mbalimbali wameandika tungo mbalimbali zinazoonyesha vile ambavyo mazingira yameharibiwa na hatimaye kuelezea kuwa kuna haja ya mazingira haya kukombolewa.

Kithaka wa Mberia (2001) katika *Bara Jingine,* ambao ni mkusanyiko wa mashairi, anaangazia matendo ya kibinadamu yanayoharibu mazingira. Katika baadhi ya mashairi kama vile "Jinamizi" (Uk. 55), "Ngao" (Uk. 59), "Mimi mto Nairobi" (Uk. 63) na Bwawa la Ithanje" (uk. 69), mwandishi huyu ameonyesha jinsi mazingira yanavyoharibiwa na hatimaye kuwahamasisha wanajamii kuwa kuna haja ya kuyatunza mazingira.

Wamitila pia amechangia swala la ukombozi wa mazingira katika riwaya yake ya *Tikitimaji*. Katika riwaya hii, vijana wanashirikiana kuyakomboa mazingira ambayo yanaangamizwa na watu wenye
ulafi.

#### 3.4.1.1.1 Nafasi ya wanawake katika ukombozi wa kimazingira

Kwa muda mrefu, barani Afrika na hata ulimwenguni kote, wanawake wamekuwa wakichukua nafasi muhimu katika kuyakomboa mazingira. Profesa Wangari Maathai ni mmoja wa wanawake walioongoza katika utunzaji wa mazingira ulimwenguni kote. Mwanamazingira huyu ndiye aliyeunda shirika la utunzi wa mazingira la "Green Belt Movement" (GBM). Alilianzisha shirika hili mwaka wa 1977 akishirikiana na shirika la "National Council of Women of Kenya" (NCWK) ili kushughulikia mahitaji ya wanawake wa vijijini ambao walilalamika kuwa vijito vyao vilikuwa vikikauka na kusababisha uhaba wa chakula.

Aidha, wanawake hawa walikuwa wakitembea masafa marefu ili kwenda kutafuta kuni za kupikia na pia miti ya kutengeneza ua. Shirika hili la GBM chini ya uongozi wa profesa Wangari Maathai liliwahamasisha wanawake wafanye kazi pamoja ili wapande miche na hatimaye kupanda miti inayoweza kushikilia mchanga, kuhifadhi maji ya mvua na hata miti hii iwape chakula na kuni huku wakipewa kiasi kidogo cha pesa kama malipo kwa kazi yao. Shirika la GBM pia liliwapa wanajamii mafunzo kuhusu elimu ya mazingira, likapigania unyakuzi wa ardhi na hata kukomesha uharibifu wa misitu kwa ajili ya ukulima.

Kwa kushirikiana na shirika la "United Nations Environmental Programme" (UNEP) katika kampeni ya upandaji wa mabilioni ya miti, miti zaidi ya milioni 51 imeweza kupandwa. Baada

ya kupokea tuzo la amani la Nobel mwaka wa 2004, hadhi yake kama mwanamazingira na hata ya GBM iliweza kupanda na kufikia kiwango cha kimataifa.

Rachael Carson, ambaye alikuwa mwanamke kutoka Uingereza pia hajaachwa nyuma katika utunzi wa mazingira. Alianzisha kampeni ya utunzaji wa mazingira kule Marekani. Kampeni yake ilihusu ukomeshaji wa matumizi ya kemikali ya "Dichlorodiphenyltrichloroethane" (DDT) ambayo yalikuwa yameenea sana kiasi cha kupunguza idadi ya wanyama asilia wakiwepo ndege. Kampeni yake ilipata ufanisi kwani matumizi ya DDT yalipigwa marufuku huko Marekani mwaka wa 1972.

Utafiti wa Sabula (2014) kuhusu nafasi ya wanawake katika uhifadhi wa mazingira katika riwaya ya *Nakuruto* na uliotumia mtazamo wa fasihi ya Ufeministi wa kiekolojia ulibainisha kuwa Ufeministi wa kiekolojia una nafasi ya kuwazindua wanawake ili kuleta ukombozi wa kimazingira. Aidha, Nakuruto ambaye ni mwanamke, aliwazindua wanajamii kupitia kwa elimu na maarifa yake ya kimazingira na hivyo basi kusababisha mapinduzi. Nadharia ya Ufeministi wa kiekolojia iliyotumiwa katika utafiti huu iliasisiwa na Francoise d' Eaubonne mwaka wa 1974 na ilibuniwa kwa ajili ya kuleta mapinduzi ya kiekolojia hasa kwa kumzingatia mwanamke.

Katika *Msururu wa Usaliti*, mwandishi ameusawiri ukombozi wa kimazingira kupitia kwa mwanamke Kage ambaye alikuwa kijana msomi. Kage amechorwa kama kielelezo cha jamii katika ukombozi wa kimazingira. Mwanamke huyu kama msomi na mhusika mkuu alianza kuonyesha hamu yake kuu ya utunzaji wa mazingira wakati alipokuwa akijaza fomu ya kujiunga na chuo kikuu. Kinyume na vijana wenzake waliopendelea kufanya kazi za utabibu na uhasibu ili wapate pesa haraka, Kage alichagua kozi za Jiografia na Botania kwa kuwa aliziona zikikaribiana na mambo ya kimazingira aliyokuwa ameyapendelea. Jambo hili lilimfanya kutofautiana na wazazi wake lakini aliushikilia msimamo wake wa awali. Kage alisema:

> "Siutaki utabibu. Sitaki maisha yangu yawe ya kuwatibu watu.
> Nataka kuyatibu mazingira ambayo watu ndio wanayoyaharibu.
> Nataka nikasomee mazingira"…"Mazingira?"Babake alimaka.
> "Naam baba, mazingira" "Mazingira gani?" mamake alifadhaika.
> (uk. 2).

Mazungumzo haya kati ya Kage na wazazi wake yanaonyesha kuwa wazazi wake hawakupendezwa katu na uchaguzi wake wa masomo, lakini aliendelea kuwaelezea faida za utunzaji wa mazingira kwa kusema:

> Miti ilishikilia ardhi kwa mizizi yake ili isichukuliwe na maji na upepo, miti pia ilisafisha hewa kwa kuondoa gesi kama vile dayoksidi na kaboni. Miti ilileta kivuli, ilitunza vyanzo vya maji na ilikuwa pambo kwenye sura ya dunia. Watu waliitia dunia madonda makuu walipoikata miti ovyoovyo (uk.2).

Hotuba iliyotolewa na Kage baada ya wanafunzi wa chuo kikuu kuandamana ili kupinga uovu wa kuharibiwa kwa msitu wa Rakau pia ilionyesha ukakamavu wake katika juhudi za kuyakomboa mazingira. Baada ya viongozi wa wanafunzi kutoa hotuba zao zilizowakashifu vikali viongozi waliohusika katika kuharibiwa kwa msitu wa Rakau, umati uliokuwepo ulipiga kelele huku ukipendekeza kuwepo kwa usawa wa jinsia katika kukilaani kitendo hiki. Aliyelengwa kuwakilisha wanawake katika hotuba hii alikuwa Kage.

Hata ingawa hakutarajia kuitwa kama mnenaji siku hiyo, alijikakamua na kutoa hotuba yake iliyowashtumu vikali viongozi wa nchi waliopewa jukumu la kutunza mazingira na mali asili ya taifa na badala yake kutumia mamlaka hayo vibaya kwa kujigawia msitu huu ambao ulikuwa chanzo cha maji yaliyokuwa tegemeo kubwa kwa wakazi wa mji mkuu. Katika kuimalizia hotuba yake, Kage alipendekeza kuundwa kwa kamati ya kukusanya miche ili iweze kupandwa katika msitu wa Rakau kama njia ya kuyakomboa mazingira hayo yaliyokuwa yameharibiwa kupitia kwa ufyekaji wa miti kwa ajili ya ujenzi.

Kage kama mwanamke aliyejitolea kuyakomboa mazingira aliendelea kupiga hatua mbele katika kazi yake kwa kuunda shirika alililoliita JEMA (Jeshi la Mazingira). Kazi yake kuu ilikuwa ni upanzi wa miche ambayo aliwagawia wananchi waweze kuipanda katika maeneo ambayo hayakuwa na miti ya kutosha bila hata kuwauzia miche hii. Gharama yote ya upanzi na utunzi wa miche hii ilikuwa juu yake. Alikuwa amejitolea kwa hali na mali katika kuyatunza mazingira. Mradi huu ulipata ufanisi mkubwa hata zaidi ya alivyotarajia Kage.

Katika kongamano la wakuu wa shule za upili jijini, Kage aliomba kualikwa ili akatoe hotuba juu ya utunzaji wa mazingira. Hotuba yake iliyowahamasisha viongozi hawa juu ya shirika la

JEMA pamoja na kazi yake iliwavutia sana. Aidha, alipokitembelea kijiji cha Itungi ambacho kilikuwa pahali pake pa kuzaliwa, aliwaenezea wakazi wa kijiji hiki habari kuhusu JEMA na kuwaomba wajiunge na shirika hilo ili waendelee kuyakomboa mazingira. Kweli, Kage alikuwa kielelezo bora katika jamii kwa upande wa ukombozi wa kimazingira.

### 3.4.1.2 Ukombozi wa kisiasa

Ukombozi wa kisiasa katika riwaya hii umegawika kuwili. Kuna harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe na kisha ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru.

#### 3.4.1.2.1 Harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe

Katika nchi nyingi barani Afrika, harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe zilihusisha kupigana vita na wakoloni ili waweze kuondoka na kuwaachia wenyeji nchi yao. Vita hivi havikuwa rahisi kwani Waafrika walikuwa na silaha duni huku wakoloni wakiwa na silaha madhubuti za kisasa. Aidha, Waafrika walikuwa wamegawanyika vikali. Kuna wale waliowasaidia wakoloni kuwapiga vita Waafrika wenzao huku wale wenginge wakionyesha umoja wao katika kumfukuza mtu mweupe. Hata hivyo, Waafrika walifanya juu chini kumwondoa mkoloni barani Afrika. Ukombozi huu ulipatikana kupitia kwa umwagikaji wa damu.

Katika riwaya hii, harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe ziliendelezwa kwa njia ya vita. Mwandishi anatuonyesha vile ambavyo Waafrika walijiingiza katika vita dhidi ya wakoloni hadi uhuru ukapatikana. Mhusika aliyechorwa akishiriki katika upiganiaji uhuru ni Mwamba aliyekuwa babake Mbogo. Vita vya upiganiaji uhuru havikuwa rahisi kwani watu walikamatwa ovyo ovyo kwa kutuhumiwa kuwa walikuwa na uhusiano na wapiganiaji uhuru ambao serikali ya kikoloni iliwaita maharamia. Haya yaliandamana na sheria ya kutotoka nje usiku. Licha ya mateso yote waliyoyapata Waafrika akiwepo Mwamba, hawakufa moyo katika juhudi zao za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe.

Kwa upande wa wapiganaji wa serikali ya kikoloni, mambo pia hayakuwa rahisi hata ingawa silaha zao zilikuwa bora. Hii ilikuwa kwa sababu walipigana na Waafrika ambao daima waliishi

msituni na kwa hivyo hawakuonekana. Kutokana na haya, juhudi za wapiganaji wa kikoloni za kuwaangamiza Waafrika hazikupata ufanisi mkubwa.

Kwa kuwa hakuna marefu yasiyokuwa na mwisho, vita vya uhuru vilifikia kilele na Waafrika wakapata uhuru. Majilio ya uhuru huu yaliwapa Waafrika matumaini makubwa na hata wale walioishi msituni kama Mwamba walirudi nyumbani ili kwenda kuyafurahia matunda ya uhuru.

Baaa ya muda, wanajamii hawa waligundua kuwa mambo hayakuwa yakienda sambamba kama walivyotarajia baada ya wakoloni kuondoka. Ukoloni mamboleo ulikuwa umeanza kuingia polepole katika jamii hii. Kutokana na hili, wanajamii hawa walilazimika kuanza awamu nyingine ya ukombozi.

**3.4.1.2.2 Ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru**

Nchi nyingi za Kiafrika zilipopata uhuru, wananchi wao walikuwa na matumaini makubwa ya kuongozwa vizuri na viongozi waliochukua hatamu baada ya wakoloni kuondoka. Baadaye, walikuja kugundua kuwa viongozi hawa walishughulika na kuyatosheleza mahitaji yao binafsi, bali sio yale ya wananchi waliowachagua. Uhuru kwa wananchi wengi haukuwa na maana. Punde tu baada ya kuyagundua haya, awamu nyingine ya ukombozi ilianza na hata hadi leo nchi nyingi za Ulimwengu wa Tatu zingali katika harakati ya kujikomboa mara ya pili kutokana na uongozi mbaya wa viongozi walio mamlakani.

Katika jamii ya *Msururu wa Usaliti*, hali sio tofauti na hii kwani baada ya uhuru, wananchi walikuja kufahamu kuwa uhuru walioupata haukuwasaidia kwa chochote kile. Kwanza, utawala ulikuwa wa chama kimoja tu kwa muda mrefu. Utawala huu uliendelea kuwakandamiza wanajamii hawa kwa muda mrefu hadi wakaonelea kuwa kulikuwa na haja ya ukombozi wa pili. Ukombozi huu ulianza kujitokeza kutokana na kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa katika jamii hii. Ni kutokana na hali hii ambapo viongozi wa vyama vya upinzani walipata nafasi ya kuwania nyadhifa mbalimbali serikalini. Mwanzoni, mfumo huu haukuwafaa viongozi wa upande wa upinzani kwa kuwa waliojitokeza kuwania viti walikuwa wengi huku wale wa chama tawala wakiwa wachache.

Kutokana na mgawanyiko huu, wanachama wote wa upinzani walipoteza nyadhifa walizokuwa wakiwania. Hali iliendelea kuwa hivi hadi pale ambapo Kage na msafara wa vijana wenzake walipokitembelea kijiji cha Itungi na kuyasikiza malalamishi ya wanakijiji kutokana na utawala mbaya wa viongozi wa chama tawala waliokuwa mamlakani. Kuanzia wakati huu, vyama vya upinzani vilipata nguvu mpya na hiki kikawa kilele cha ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru.

**3.4.1.2.2.1 Nafasi ya vijana katika ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru**

Katika mataifa mengi barani Afrika na hata nje ya bara, vijana huwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa wakati wa uchaguzi mkuu. Kampeni nyingi za kisiasa huhudhuriwa sana na vijana ambao huwa wana ufungamano mkubwa na wagombea viti katika viwango mbalimbali. Vijana hawa hutumiwa na wagombea viti katika kuwaelimisha wananchi juu ya upigaji kura na hata kuwafanyia kampeni wagombeaji wao hadi mashinani.

Katika *Msururu wa Usaliti*, vijana wasomi wamechukua nafasi kubwa katika kuuvunjilia mbali mfumo wa utawala wa chama kimoja. Mwandishi amewatumia vijana wa kike na kiume katika kuuleta ukombozi wa pili kwa wanajamii. Vijana hawa walikuwa mhusika mkuu Kage, Agutu aliyekuwa mwanasheria, Daktari Makau na Kanali Upepo.

Mabadiliko haya yalianza kufanyika wakati ambapo Kage na vijana wenzake walialikwa katika kijiji cha Itungi na mamake Sarah. Sarah alikuwa mfanyikazi wa Kage aliyempenda sana. Kage alipokubali wito huu, maandalizi yote yalifanywa kijijini ili kuwapokea wageni hawa. Kijiji chote kilikusanyika kwa Naito aliyekuwa mamake Sarah. Siku ilipofika, wageni hawa walilakiwa na kijiji kizima na baada ya karamu murua kuandaliwa, wanakijiji hawa waligawika katika makundi huku kila mmoja wa wasomi hawa akijiunga na kundi lake.

Kutokana na mazungumzo ya kina, wanakijiji hawa walifichua shida zilizokuwa zikiwakabili kutokana na uongozi mbaya wa chama tawala. Kwa mujibu wa Marx katika nadharia yake ya U-Marx katika Wamitila (2006:182-184), njia ya kusaidia na labda kuharakisha kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushtumu, kulaumu na kufichua batili iliyopo katika itikadi za kibwanyenye inayouimarisha ubepari. Ufichuzi huu ndio uliopelekea katika juhudi za kuanza kuuvunja mfumo wa kibepari wa chama tawala.

Wakati huu, kinyume na zamani, Kage alionyesha kuvutiwa na mambo ya kisiasa. Haya yaliandamana bega kwa bega na kupoteza kiti cha ubunge kwa Mbogo aliyekuwa mbunge wa Rware na babake Kage. Tukio hili lilisababishwa na Mbogo kuhukumiwa kifungo cha jela kwa kushiriki katika mauji ya mke wake, Makena. Ilikuwa wazi kuwa uchanguzi mdogo ungefanywa ili kuijaza nafasi ya Mbogo.

Shida za wanakijiji wa Rware zilipelekea kuundwa kwa chama cha kisiasa cha UWATA (Umoja wa Wazalendo wa Taifa). Kwa sauti moja, wanakijiji hawa walimshinikiza Kage agombee kiti cha ubunge cha Rware kwa tiketi ya UWATA, jambo ambalo hakulipinga. Kutokana na uchaguzi mdogo huo, chama cha UWATA kilipata ushindi mkubwa dhidi ya wapinzani wao wa chama tawala. Huu ndio uliokuwa mwamko mpya wa mabadiliko katika jamii hii. Aidha, kutokana na ushindi wa Kage, taifa jipya lilizaliwa na wananchi wakawa na matumaini makubwa ya kupata ukombozi zaidi.

#### 3.4.1.3 Ukombozi dhidi ya ufisadi

Katika mataifa mengi ya Ulimwengu wa Tatu, ufisadi umekithiri na ndio chanzo cha uchumi wa nchi nyingi kuporomoka na kuzorota. Katika mataifa haya, kesi nyingi za ufisadi zinahusisha uporaji na upoteaji wa fedha za umma. Fedha hizi huwa zimetengewa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali za nchi na zinapopotea, miradi hii haitekelezwi na hivyo basi, kusababisha uchumi kudidimia.

Katika riwaya hii, mwandishi ameisawiri picha ya nchi iliyokumbwa na ufisadi unaoendelezwa na watu wa tabaka la juu. Ardhi inanyakuliwa na viongozi. Vilevile, viongozi wa upinzani wananunuliwa na viongozi wenzao kutoka chama tawala. Msanii wa riwaya hii ameuendeleza ukombozi dhidi ya ufisadi kupitia kwa vijana wasomi.

##### 3.4.1.3.1 Nafasi ya vijana katika ukombozi dhidi ya ufisadi

Katika ujenzi wa taifa lolote, vijana huchukua nafasi fulani kwa kuwa wao ndio hutarajiwa kuwa viongozi wa siku zijazo. Kwa hivyo, kuna haja kubwa ya kuwa na vijana walioelimika ili waweze kuwa viongozi wa kutegemewa siku za usoni.

Katika *Msururu wa Usaliti*, jamii inakombolewa dhidi ya ufisadi na vijana wasomi. Mwandishi anawahusisha vijana Kage, Nafula na Daktari Makau katika ukombozi huu. Shughuli yote ya ukombozi inaanzishwa na Kage kabla ya kuwahusisha wenzake. Ujasiri wa Kage hauna kifani kwa kuwa anayatekeleza mambo yake bila kumwogopa yeyote. Yeye ni kinyume na wanajamii wengi kwa kuwa wengi wao walishuhudia maovu mengi yakitendwa lakini hawangethubutu kuyasema kwa hofu ya kuchukuliwa hatua na serikali tawala kwani mengi ya maovu haya yalitekelezwa na viongozi wakuu serikalini.

Kage alikuwa amepewa kipande cha ardhi cha kuotesha miche na Kipanga aliyekuwa mmoja wa matajiri wakubwa nchini. Baada ya mazungumzo na diwani mmoja wa upinzani, Kage alikuja kugundua kuwa ardhi aliyopewa na Kipanga ili kuendeleza shughuli ya uhifadhi mazingira haikuwa yake, bali ilikuwa ardhi ya umma. Diwani huyu alikuwa na ithibati zote zilizoonyesha kuwa ardhi hii ilikuwa imenyakuliwa kutoka Halmashauri ya jiji na kuhamishiwa mikononi mwa Kipanga. Diwani huyu alimkabidhi Kage karatasi zote na kumhakikishia kuwa angemtafutia mengine ya kuthibitisha unyakuzi zaidi wa mali ya umma.

Bila kusita, Kage alimtafuta Kipanga na kumwelezea vile ambavyo alikuwa amenyakua ardhi ya umma. Jambo hili lilimshangaza na kumgadhabisha sana Kipanga asijue la kufanya. Kage alikuwa tayari kuufichua uovu huu kwa umma na kwa hivyo alimwendea wakili Nafula kwa ushauri. Alimwonyesha Nafula ithibati zote naye akamhakikishia kuwa alikuwa amelindwa kisheria katika kuyatangaza mambo haya. Wasiwasi wa Nafula ulikuwa mmoja tu; kwamba wanyakuzi hawa walikuwa watu hatari na wa kuogopewa. Kage kwa upande wake alimhakikishia kuwa hakuogopa chochote kwa kusema: “Mimi siogopi.” Kage alisema. “Kwani watanifanya nini?” (uk. 165).

Hatua iliyofuata ilikuwa kumhusisha Daktari Makau katika jambo hili na kisha wote watatu waliandika ripoti kuhusu unyakuzi huu na ambayo waliisoma mbele ya waandishi wa habari. Baada ya usomaji, habari hizi zilienea kila upande wa nchi kupitia kwa vyombo vya habari kama vile redio, runinga na hata magazeti.

Kitendo hiki cha ujasiri kiliwafungua macho wananchi wengi kwa kuyafahamu maovu yaliyokuwa yakiendelezwa serikalini. Pamoja na haya, waliwapongeza wazalendo hawa kwa kazi yao nzuri kwa kuandamana katika barabara za mji mkuu huku wakiimba nyimbo za kuwasifu watatu hawa. Hatimaye, Kipanga na maofisa wawili wa idara ya usajili wa mashamba walishikwa na kushtakiwa kwa kosa la kushirikiana katika kuiba ardhi ya Halmashauri ya jiji.

Baada ya muda, majaribio ya kumwua Kage kutokana na kitendo chake cha ujasiri na uzalendo yalifanywa kupitia kwa gari lake kupigwa risasi kadhaa lakini hayakufua dafu. Mambo yaliporudia hali ya kawaida, Kage aliendelea kuonyesha ushupavu wake wa ukombozi kwa kutuma ombi la kupewa rasmi ile ardhi iliyokuwa imenyakuliwa ili aweze kuiendeleza kazi yake ya upanzi wa miche chini ya shirika la JEMA. Ombi lake lilikubaliwa bila tashwishi yoyote na hata maofisa waliohusika wakampongeza kwa juhudi zake za kuikomboa ile ardhi.

#### 3.4.1.4 Ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa

Kwa muda mrefu, mataifa ya ulimwengu wa tatu yameendelea kukumbwa na viwango vya juu vya umaskini. Utafiti uliofanywa na shirika la United Nations Childrens' Education Fund (UNICEF) ulibainisha kuwa watu takribani milioni 18 hufa kila mwaka kwa sababu zinazohusiana na umaskini. Kwa jumla, watu milioni 270, wengi wao wakiwa wanawake na watoto, wamefariki kutokana na umaskini tangu mwaka wa 1990. Watu wanaoishi katika hali ya umaskini huteseka kwa viwango visivyo sawa kutokana na njaa au hata magonjwa.

Kulingana na shirika la afya duniani (WHO), njaa na ukosefu wa lishe bora ndilo tishio kuu kwa afya ya umma duniani na ukosefu wa lishe bora ndio unaochangia pakubwa vifo vya watoto. Kila mwaka, karibu watoto milioni 11 wanaoishi katika umaskini hufa kabla ya kufikisha miaka mitano. Kulingana na utafiti wa shirika hili, watu bilioni 1.2 hulala bila chakula kila siku.Mojawapo kati ya njia bora zaidi za kupunguza umaskini katika nchi yoyote ile ni kuhakikisha kuwa haki ya maskini ya kumiliki mali imelindwa. Ulindaji wa haki ya kumiliki ardhi, ambayo ni rasilmali kubwa zaidi katika jamii nyingi, ni muhimu katika kuhakikisha uhuru wa kiuchumi.

Wanajamii wa *Msururu wa Usaliti* wamekumbwa na umaskini na hata magonjwa yanayotokana na umaskini huu. Mwandishi amewatumia wahusika kuonyesha juhudi za kuangamiza umaskini na magonjwa katika jamii hii. Msanii wa riwaya hii amemsawiri Mbogo kama mtoto maksini baada ya kufiwa na wazazi wake wote kutokana na vita vya kujikomboa kutokana na ukoloni mkongwe. Jamaa zake pia walimtupa na hawakuweza kumsaidia kwa njia yoyote.

Baada ya kuwaza kwa muda juu ya vile ambavyo angeweza kuyaendeleza maisha yake na kujinasua kutokana na baa la umaskini, Mbogo anaamua kwenda kutafuta ajira katika ranchi ya Bwana Mark, aliyekuwa mmoja wa masetla ambao hawakuondoka baada ya uhuru. Bwana Mark anamkubali na kumpa kazi ya kuchunga na kukamua ng'ombe. Hali ya maisha yake inaanza kubadilika kwani kwa mara ya kwanza anakula na kushiba, analala usingizi mnono na hata kulipwa vizuri.

Mbogo anaendelea na kazi yake huku akijiwekea akiba kidogo kidogo. Baada ya miaka mitatu, ndoto ya utajiri inaanza kumjia na ni wakati huu ambapo alianza kufikiria juu ya kilimo cha mibuni. Ndoto yake inampeleka kwa Igweta aliyekuwa na sehemu ya ardhi aliyokuwa imepandwa mibuni na kumsihi amwuzie kipande cha ardhi hii. Igweta analikubali ombi la Mbogo na kumwuzia ekari tatu za ardhi yake.

Kuanzia wakati huu, Mbogo anajiuzulu kazini kwa Bwana Mark na kuanza kilimo cha kahawa. Mapato kutokana na kilimo hiki yanamfanya aendelee kupaa zaidi na kuuaga umaskini. Baada ya miaka miwili, alikuwa mkulima aliyesifika kijijini kote. Ndoto yake ya maisha inatimia na ukombozi kamili dhidi ya umaskini unapatikana kwake. Hali ya kuwa na pesa nyingi ndiyo inayomfanya ajiingize katika harakati za kisiasa za kuwania kiti cha ubunge wa Rware. Mbogo aliyeachwa bila chochote na wazazi wake anapaa na kuwa Mbogo milionea.

Daktari Makau kama kijana msomi anajiingiza katika harakati za kuwakomboa wananchi kutokana na magonjwa ambayo wanakijiji hawa hawangeweza kuyamudu kutokana na umaskini.

#### 3.4.1.4.1 Nafasi ya vijana katika ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa

Ili kupata maendeleo katika nchi, vijana wanafaa kuelimishwa ili waweze kuwa matabibu wa siku za usoni na hivyo basi kuwakomboa wanajamii kutokana na magonjwa ambayo wakati mwingine husababishwa na umaskini.

Katika *Msururu wa Usaliti*, mwandishi amemchora Daktari Makau kama kielelezo cha uzalendo katika jamii.  Kwanza, mhusika huyu amesawiriwa kama kijana tofauti na wengine kwa kuwa wengi wa waliokuwa na elimu ya kuwawezesha kuwa matabibu walianzisha kliniki zao binafsi huku wakiwa wameajiriwa katika hospitali za umma kwa tamaa ya kujipatia fedha nyingi. Daktari huyu hakufanya hivi kwa kuwa alitaka kuutumia wakati wake wote wa kazi katika kuwahudumia wagonjwa kwa njia ifaayo.

Baada ya kugundua kuwa wananchi wengi walikuwa wakisumbuliwa na magonjwa huko vijijini kutokana na hali ya umaskini iliyowakabili, Daktari Makau anapanga msafara wa kwenda kutoa huduma za matibabu ya bure mashambani humo. Hata ingawa kulikuwa na shida ya usafiri na uhaba wa madaktari na wauguzi, Daktari huyu anafanya juu chini kuhakikisha kuwa amepata madaktari na wauguzi wa kumsaidia katika kazi hii na hatimaye kutafuta gari la kuwasafirisha hadi mashambani.

Maandalizi yote yanapokamilika, Daktari Makau anahakikisha kuwa wanakijiji wamepashwa habari juu ya huduma za matibabu mashambani kupitia kwa redio ya taifa. Walinuia kutembelea maeneo ya Rware, Itungi na Ntue mtawalia. Siku ya kwanza wanapofika Rware, wanapata halaiki ya watu ikiwangojea kwa hamu ili iweze kupata matibabu ya bure. Wanafanya kazi hadi usiku na kukosa kuwahudumia wagonjwa wote.

Jambo lililowashangaza wahudumu hawa ni hali ya umaskini uliokithiri kiasi cha wagonjwa waliopimwa na kupatikana na kifua kikuu kukosa matibabu kwa ukosefu wa fedha. Siku ya pili na ya tatu, hali ya wingi wa wagonjwa waliohitaji matibabu ilikuwa haipungui. Hata hivyo walijikakamua na kuwahudumia wagonjwa wote.

#### 3.4.1.5 Ukombozi dhidi ya uozo wa jamii

Katika nchi nyingi barani Afrika na hata ulimwengu mzima, uozo wa jamii umekuwa ukipewa kipaumbele katika vyombo vya habari kila uchao. Mauaji, ubakaji, uasherati na uzinzi vinapiga vichwa vya habari katika magazeti kila siku. Haya ni mambo ya dharura ambayo jamii inahitaji kukombolewa dhidi yake.

Jamii ya *Msururu wa Usaliti* imetia juhudi katika kujikomboa dhidi ya uozo wa jamii kama vile mauaji, ubakaji na usherati na uzinzi.

##### 3.4.1.5.1 Ukombozi dhidi ya mauaji

Mauaji ya watu wasio na hatia katika nchi mbalimbali yameshuhudiwa. Mwaka wa 1994, mauaji ya halaiki ya watu yalishuhudiwa nchini Rwanda na Burundi. Makabila ya Hutu na Tutsi yaliuana bila huruma. Hatimaye nchi hizi zilikombolewa kutokana na mauaji haya na hali ya kawaida ikarudiwa.

Katika riwaya hii, Kage anaendeleza ukombozi dhidi ya mauaji. Mama yake Kage alikufa kwa njia ambayo Kage hakuielewa alipokuwa masomoni Uingereza. Baada ya kuhudhuria mazishi na kurudi masomoni, kage alituhumu kuwa kifo cha mamake hakikuwa cha kawaida na kuamua kuwa angefanya uchunguzi kamili baada ya kuyamaliza masomo yake na kurudi nchini.Ukweli wa kifo cha mamake ulimfikia Kage baada ya kusimuliwa kisa na mfanyikazi wake Sara. Sarah alizipata habari hizi kutoka kwa rafiki yake aliyekuwa mhudumu katika klabu. Ni katika klabu hiki ambapo Mbogo aliyekuwa mumewe Makena na babake Kage alifanyia mipango ya kumwua mke wake akiwa na mfanyikazi wake Mdudu.

Ukweli ulipowekwa wazi, Kage aliamuru kukamatwa kwa babake na kutiwa ndani ili amfunze adabu kutokana na kitendo hiki kiovu. Mdudu na rafiki yake Sara pia walitiwa ndani kuhusiana na kifo cha mamake Kage. Mbogo alitumikia kifungo cha maisha na kupoteza kiti chake cha ubunge wa Rware. Kitendo cha ujasiri cha Kage kilikuwa cha kuwaonya wale wengine waliokuwa na nia ya kushiriki katika vitendo viovu kama hivi.

### 3.4.1.5.2 Ukombozi dhidi ya ubakaji

Kila uchao, visa vya ubakaji huripotiwa katika vyombo vya habari. Ajabu ni kuwa watoto wenye umri mdogo sana ndio hushirikishwa katika kitendo hiki. Sheria mpya zinazidi kuundwa ili kukomesha maovu haya lakini hazifuatwi.

Katika riwaya ya *Msururu wa Usaliti*, Mbogo anambaka mfanyikazi wao wa nyumbani na kukiweka kitendo hicho kama siri moyoni mwake huku naye msichana akitorokea kwa wazazi wake. Jambo hili linamkera Makena kwa kuwa mumewe alishiriki katika vitendo vingi vya uasherati lakini hakuwahi kumchukulia hatua yoyote kwa kuogopea kuwa ndoa yao ingevunjika na mtoto wao Kage kutopata malezi na upendo ufaao kutoka kwa wazazi wake. Kulingana na Makena, huu ulikuwa usaliti mkubwa zaidi aliowahi kufanyiwa na mumewe maishani mwake.

Mara nyingi, visa vya aina hii huwekwa kama siri kuu kwa ajili ya kuogopa aibu na gharama. Kwa Makena, mambo yalikuwa tofauti kwani mwandishi ameusawiri ukombozi dhidi ya ubakaji kupitia kwake. Makena alimsaidia msichana huyu kupelekwa hospitali na ithibati ya ubakaji kupatikana. Baada ya shughuli nzima, Makena anashinikiza mumewe kushikwa na kuwekwa ndani ili apate adabu. Aidha, anahakikisha kuwa mumewe analipia gharama ya uharibifu huu kwa shilingi laki tano. Mbogo hakuwa na lingine la kufanya ila kuifidia jamii ya mfanyikazi wao ili asikae ndani na kukipoteza kiti chake cha ubunge. Hili halikuwa funzo kwa Mbogo peke yake, bali kwa wengine waliokuwa na mienendo kama yake.

### 3.4.1.5.3 Ukombozi dhidi ya uasherati na uzinzi

Uasherati na uzinzi ni kosa ambalo limezifanya familia nyingi kutengana huku watoto wasio na hatia wakiachwa kuteseka. Njia ya pekee ya kujikomboa kutokana na uozo huu katika jamii ni watu kuwa waaminifu katika ndoa.

Katika *Msururu wa Usaliti*, ukombozi wa aina hii unaendelezwa kupitia kwa wahusika Daktari Makau na Nafula. Nafula alikuwa mpenzi wa zamani wa Daktari huyu. Baada ya Nafula kwenda masomoni ng'ambo, Daktari Makau alionelea kuwa asingeweza kumngojea amalize masomo yake ndipo waweze kuoana. Wakati wa kurudi nchini, alimpata mpenzi wake akiwa bado hajaoa lakini alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Agutu aliyedhamiria kumwoa. Agutu alikuwa

msherati na mzinzi lakini Daktari Makau hakulifahamu jambo hili. Wakati huu, Agutu alikuwa ameambukizwa virusi vya ukimwi.

Nafula anamkomboa Daktari Makau kutokana na uasherati wa Agutu kwa kumfichulia ukweli juu ya tabia zake. Nafula anamsimulia Daktari huyu habari zote juu ya vile ambavyo Agutu alishiriki katika kulewa akiwa na Kipanga. Anapojua ukweli wa mambo na kuhakikisha kuwa hakuwa mgonjwa kupitia kwenda kupimwa, Daktari Makau anasahau mambo ya Agutu na kurudiana na Nafula kisha wanafanya arusi iliyofana sana.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura ya tatu, tulishughulikia swala la ukombozi katika *Msururu wa Usaliti*. Tulizichanganua changamoto zinazoikumba jamii hii zikiwepo uharibifu wa mazingira, ukoloni, ufisadi,uongozi mbaya, umaskini, utabaka na uozo wa jamii.

Uharibifu wa mazingira ulipelekea kukatwa kwa miti katika msitu wa Rakau na hivyo basi, visima kukauka. Ukoloni nao umegawanyika kuwili ambapo kuna ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Ufisadi kwa upande mwingine uliiharibu jamii husika kupitia unyakuzi wa ardhi na kununuliwa kwa wabunge na madiwani wa upinzani. Umaskini nao umewafanya wanajamii kutokwenda kupata matibabu dhidi ya magonjwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Aidha, utabaka katika jamii hii ndio umeanzisha mfumo wa ubepari ambapo viongozi wamo katika tabaka la juu huku wananchi wakiwa katika tabaka la chini. Uongozi mbaya katika jamii hii unawafanya wananchi kudhulumiwa na viongozi wanaoyajali maslahi yao pekee. Uozo wa jamii nao umehusisha mauaji, ubakaji na usherati na uzinzi. Maovu haya yametekelezwa na viongozi pamoja na wananchi.

Vilevile, tulizichanganua aina tofauti za ukombozi katika riwaya hii. Ukombozi huu unatokana na changamoto tulizozielezea. Ukombozi tuliouzungumzia ni ukombozi wa kimazingira, ukombozi wa kisiasa, ukombozi dhidi ya ufisadi, ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa kisha ukombozi dhidi ya uozo wa jamii. Katika ukombozi wa kimazingira, Kage kama mwanamke na pia mhusika mkuu ameuendeleza ukombozi huu. Ukombozi wa kisiasa nao umegawanyika katika harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe, kisha ukombozi wa

kisiasa baada ya uhuru. Vijana wasomi na wazalendo waliojiita wazaliwahuru wamechukua nafasi ya kwanza katika ukombozi huu wa kisiasa. Vijana hawa pia wameongoza katika kuikomboa jamii dhidi ya ufisadi wakiongozwa na Kage. Ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa umeendelezwa na Daktari Makau huko mashambani ambamo kuna visa vingi vya magonjwa kutokana na umaskini.

Ukombozi dhidi ya uozo wa jamii nao umegawanyika katika ukombozi dhidi ya mauaji, ukombozi dhidi ya ubakaji na kisha ukombozi dhidi ya uasherati na uzinzi. Ukombozi huu umeendelezwa na Makena aliyekuwa mamake Kage, Kage mwenyewe na **N**afula**.**

Kwa jumla, mwandishi wa riwaya hii amewasawiri vijana wa kike na wa kiume kama vielelezo vya kuikomboa jamii husika kutokana na madhila yanayoikabili. Msanii huyu ametuchorea picha ya taifa jipya ambalo limezaliwa kutokana na ushirikiano na juhudi za vijana hawa. Aidha, katika kazi hizi, Mwenda Mbatiah ameihamasisha jamii husika na wasomi wote kwa jumla juu ya umuhimu wa elimu. Ni kutokana na hali ya kuelimika ambapo vijana hawa wamepata ujuzi wa kutosha wa kuikomboa jamii kwa njia ya haki bila kusababisha ugomvi kati ya wanajamii.

# SURA YA NNE
# MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa matokeo kutokana na uchunguzi wetu. Tumekusudia kubainisha iwapo madhumuni ya utafiti wetu yameafikiwa. Tumefanya hivi kupitia kwa kuzipima nadharia tete za utafiti wetu na hata tukatoa mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye kuhusiana na mada yetu.

## 4.2 Muhtasari wa matokeo

Katika utafiti wetu, tumeshughulikia riwaya mbili za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* za Mwenda Mbatiah. Tumetumia nadharia ya U-Marx kuchanganua maudhui ya ukombozi katika riwaya hizi mbili. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni matatu. Kwanza, tulitathmini changamoto zinazozikumba jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Utafiti wetu ulibainisha kuwa jamii hizi mbili zimekumbwa na changamoto nyingi. Jamii ya *Wimbo Mpya* imekumbwa na changamoto kama vile ukoloni, ukosefu wa elimu, utabaka, mvutano baina ya usasa na ukale na dhuluma dhidi ya wanawake.

Ukoloni katika jamii ya *Wimbo Mpya* umegawanyika katika ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Ukoloni mkongwe katika jamii hii ulihusisha Waafrika kutawaliwa na wakoloni Waingereza. Waafrika waliupoteza uhuru wao na kuwa chini ya sheria za wakoloni. Ukoloni mkongwe ulikuwa na athari zake kama vile mgawanyiko wa jamii katika makundi ya wazalendo na wasaliti. Ukoloni mamboleo nao uliingia baada ya uhuru kupatikana. Waafrika waligundua kuwa uhuru waliokuwa wameupata kutoka kwa wabeberu ulikuwa wa bendera tu, hivyo basi wakaendelea kuthibitiwa kiuchumi na kisiasa. Kutokana na haya, iliwabidi Waafrika kuanza kujikomboa mara ya pili. Kwa upande mwingine, ukosefu wa elimu uliwafanya wanajamii kuachwa nyuma katika shughuli za kimaendeleo. Changamoto hii ilitokana na hali kuwa shule zilikuwa chache na pia zilikuwa mbali kiasi cha kutofikika kwa urahisi. Isitoshe, Waafrika hawakufahamu umuhimu wa kuwa na elimu.

Utabaka nao ni changamoto ambayo iliifanya jamii ya *Wimbo Mpya* kugawanyika katika makundi ya watu wa tabaka la juu na la chini na hata wenye elimu na wasio na elimu. Mvutano baina ya usasa na ukale umesawiriwa kupitia kwa mazungumzo baina ya Mwathi na Yohana Nthambori. Mwathi ameshikilia ukale huku naye Nthambori akishikilia usasa. Haya yanaonekana katika mazungumzo yao wanapokunywa pombe ya kienyeji ambayo Mwathi anaonelea kuwa ndiyo bora zaidi huku naye Nthambori akionelea kuwa pombe ya kisasa na inayonywewa kwenye mabaa ndio bora zaidi.

Dhuluma dhidi ya wanawake pia ni changamoto nyingine inayoikumba jamii hii. Bi. Mariamu ni mmoja wapo wa wanawake wanaodhulumiwa na wanaume. Anatendewa haya na bwanake kwa sababu ya kuwa tasa na hata mwishowe anampa talaka. Vilevile, kakake Bi. Mariamu kwa jina Yohana Nthambori anamdhulumu kwa kutomrithisha chochote baada ya kifo cha baba yao kwa kudai kuwa mila na desturi hazikumruhusu mwanamke kurithi mali. Aidha, mwanamume huyu pia alimdhulumu Bi. Mariamu kwa kumfukuza kutoka kwa nyumba ya baba yake alimokuwa akiishi kwa madai kuwa alitangamana na watu wa kijijini ambao walikuwa maskini.

Kwa upande mwingine, jamii ya *Msururu wa Usaliti* imekumbwa na changamoto nyingi zikiwepo uharibifu wa mazingira, ukoloni, ufisadi, umaskini, uozo wa jamii, utabaka na uongozi mbaya. Katika jamii hii, mazingira yameharibiwa kupitia kwa ufyekaji misitu unaoongozwa na viongozi wakuu serikalini. Ukoloni katika jamii hii sio tofauti na ule ulio katika *Wimbo Mpya*. Ukoloni huu pia umegawanyika katika ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Ukoloni mkongwe ulihusisha harakati za kupigana vita kati ya Waafrika na wakoloni hadi uhuru kupatikana. Uhuru uliopatikana ulikuwa wa bendera tu, hivyo basi ukombozi wa pili unaanza ili uhuru kamili upatikane.

Ufisadi unaendelezwa kupitia kwa unyakuzi wa ardhi ya umma. Ufisadi huu unahusisha viongozi wakuu serikalini na hata kiongozi wa nchi mwenyewe. Umaskini nao umekithiri katika jamii ya *Msururu wa Usaliti* ambapo wanajamii hawawezi kwenda kupata huduma za matibabu kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Uozo wa jamii nao unahusisha mauaji, ubakaji, uasherati na uzinzi. Watu wasio na hatia kama vile Makena waliuawa. Vilevile, mfanyikazi wa Makena

alibakwa na mumewe kwa jina Mbogo. Kwa upande mwingine, watu kama Agutu, Mbogo, Kipanga na Owawa wanaendeleza uasherati na uzinzi katika jamii hii.

Changamoto ya utabaka imedhihirika ambapo jamii imegawanyika katika matabaka ya watawala na watawaliwa, matajiri na maskini na kisha wenye elimu na wasio na elimu. Uongozi mbaya nao unawafanya viongozi kuyajali maslahi yao binafsi bila kuwajali wananchi waliowatawala.

Madhumuni ya pili yalikuwa kuchunguza aina tofauti za ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Kulingana na mihimili ya nadharia ya U-Marx, Ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali kutokana na juhudi za wafanyikazi au wenyewe utaishia kujiangamiza kutokana na mbegu za maangamizi unazozisheheni. Katika jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*, wanajamii wameingilia kati na kuanza juhudi za kujikomboa ili kuuvunjilia mbali mfumo wa ubepari katika jamii hizi. Aina za ukombozi tulizozichunguza ni ukombozi wa kimazingira, ukombozi wa kisiasa, ukombozi dhidi ya ufisadi, ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa, ukombozi dhidi ya uozo wa jamii, ukombozi wa kielimu na ukombozi wa kiuchumi.

Utafiti huu ulibainisha kwamba vijana wa kike na wa kiume na hata wanawake wamechukua nafasi kubwa katika kuzikomboa jamii hizi mbili. Katika *Wimbo Mpya*, Bi. Mariamu kama mwanamke amesawiriwa kama kielelezo cha jamii katika kuikomboa jamii husika kielimu na kiuchumi. Mwanamke huyu anajihusisha katika shughuli ya ujenzi wa shule na anafaulu hata ingawa alikuwa mgeni kijijini na hakuwa ametangamana na wanakijiji wengi. Ujasiri na ukakamavu wake ndio uliomfanya afaulu katika kuikomboa jamii kielimu. Aidha anawaleta akina mama pamoja na kuanza mradi wa kujiendeleza kiuchumi.

Katika *Msururu wa Usaliti*, vijana wasomi waliojiita wazaliwahuru ndio walioongoza katika kuikomboa jamii katika viwango tofauti tofauti. Kage kama kijana asiyeshawishika na maoni ya wengine anajishirikisha katika kuikomboa jamii kwa upande wa mazingira kupitia kwa upanzi wa miti. Aidha, Kage, Agutu, Daktari Makau na Kanali Upepo kama vijana wamesawiriwa kama vielelezo vya jamii ya *Msururu wa Usaliti* kwa kushiriki katika ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru. Vijana hawa wanashiriki katika kuuvunjilia mbali utawala wa chama kimoja na kuanzisha

mfumo wa vyama vingi. Ni kufuatia mfumo huu ambapo chama cha UWATA kinashinda uchaguzi mdogo wa eneo bunge la Rware chini ya uongozi wa Kage kama mbunge mpya. Kuanzia wakati huu, taifa jipya linazaliwa na mabadiliko yaliyokusudiwa kupatikana.

Aidha Kage, Nafula na Daktari Makau walijiingiza katika kuikomboa jamii dhidi ya ufisadi kupitia kwa ufichuzi wa ardhi iliyonyakuliwa na Kipanga na habari kuenezwa kupitia kwa vyombo vya habari. Daktari Makau naye kama kijana anaikomboa jamii kutokana na umaskini na magonjwa kwa kupanga msafara wa kwenda kupeana matibabu ya bure kule mashambani. Vilevile, Kage na Agutu kama vijana wanashiriki katika kuikomboa jamii kutokana na uozo wa jamii. Kage anafichua mauaji ya kinyama yaliyofanyiwa mamake na Mdudu akishirikiana na Mbogo aliyekuwa babake. Aidha, Nafula anafichua uasherati na uzinzi uliokuwa ukiendelezwa na Agutu aliyekuwa mpenziwe Daktari Makau. Kwa kufanya hivi, anamkomboa Daktari huyu kutokana na janga la UKIMWI ambalo lilikuwa limempata Agutu na hata kusababisha kifo chake. Makena naye aliyekuwa mkewe Mbogo anashiriki katika kuikomboa jamii kutokana na ubakaji kwa kuhakikisha kuwa mumewe aliyembaka mfanyikazi wao wa nyumbani amechukuliwa hatua kali za kisheria.

Madhumuni ya tatu yalikuwa kuonyesha mikakati ya kujikomboa wanayoitumia wanajamii wa *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Utafiti huu ulionyesha kuwa wanajamii hawa walibuni mikakati ya kujikomboa kama vile uundaji wa majeshi ya vita ya kupigania uhuru, uundaji wa vyama vya kisiasa kama vile UWATA ili kuwaunganisha wanajamii, kuanzishwa kwa shirika la utunzaji wa mazingira lililojulikana kama JEMA, ujenzi wa shule ili kujikomboa kielimu, kuanzishwa kwa vikundi vya akina mama vya kujiendeleza kiuchumi na hata kupeleka huduma za matibabu vijijini bila malipo.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete tatu. Nadharia tete ya kwanza ilikuwa “Kazi za Mbatiah za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* zimefaulu katika kuonyesha chanzo cha vita vya ukombozi katika jamii hizi mbili.” Utafiti huu ulibainisha kuwa kazi hizi zimefanikiwa katika kuonyesha mwanzo wa vita hivi. Katika riwaya zote mbili imebainika kuwa chanzo cha vita vya ukombozi ni changamoto zilizowakumba wanajamii hawa hadi wakajiingiza katika harakati za kujikomboa.

Tumezitathmini changamoto zilizoikumba jamii ya *Wimbo Mpya* katika sura ya pili huku tukizitathmini changamoto zilizoikumba jamii *ya Msururu wa Usaliti* katika sura ya tatu.

Nadharia tete ya pili ilikuwa "Jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* zitafanikiwa katika harakati zao za ukombozi wa aina tofautitofauti." Kuhusu nadharia tete hii, utafiti wetu ulibainisha kuwa jamii hizi mbili zilifanikiwa kwa kiwango kikubwa katika harakati zao za kujikomboa. Kage alifaulu katika kuikomboa jamii *ya Msururu wa Usaliti* kimazingira. Hili aliliafikia kupitia kwa kulianzisha Shirika la JEMA ambalo lilijishughulisha na upandaji na usambazaji wa miche kwa wanajamii. Miche hii ilikua na kuyapa mazingira yaliyokuwa yameharibiwa sura mpya.

Bi. Mariamu alifaulu katika kuikomboa jamii ya *Wimbo Mpya* kielimu na kiuchumi. Kuhusu elimu, mwanamke huyu alifanya juhudi za kujenga na kuanzisha shule ya msingi kijijini mwao ambapo wanakijiji walihamishia watoto wao na kuweza kupata huduma za masomo karibu na wao kinyume na awali ambapo wanafunzi wangesafiri mwendo mrefu kwenda shuleni kwa kuwa shule zilikuwa mbali na pia zilikuwa chache. Vilevile, kuhusu ukombozi wa kiuchumi katika jamii hii, Bi. Mariamu aliliongoza kundi la wanawake la kijijini Gaito katika kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi ambayo iliwapa fedha nyingi kiasi cha kuwa na akaunti ya benki ya kikundi hiki iliyokuwa na shilingi zaidi ya elfu hamsini.

Katika jamii hizi mbili, harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni mkongwe zilifaulu kwa kuwa wanajamii hawa walijiingiza katika juhudi za kupigana vita dhidi ya wakoloni hadi wakoloni hawa wakawapa uhuru na kuondoka. Aidha, Vijana wasomi walifaulu katika kuikomboa jamii ya *Msururu wa Usaliti* kisiasa baada ya uhuru. Jambo hili lilitimizwa kupitia kwa wasomi hawa kuunda chama cha upinzani cha UWATA huku wakiungwa mkono na wanavijiji. Chama hiki kilishiriki katika uchaguzi mdogo wa eneo bunge la Rware chini ya uongozi wa Kage kama mgombea kiti. Chama hiki kilipata ushindi mkubwa katika uchaguzi huo na kuanzia wakati huo, mabadiliko yakatokea na maendeleo zaidi yakaanza kupatikana.

Vilevile, Daktari Makau alifaulu kwa kiwango kikubwa katika kuikomboa jamii ya *Msururu wa Usaliti* kutokana na umaskini na magonjwa. Alifanya hivi kwa kupanga msafara wa kwenda

mashambani ili kuwapa huduma ya matibabu ya bure wanakijiji waliokuwa wamelemewa na umaskini kiasi cha kutopata fedha za kununua dawa hata baada ya kupimwa na kupatikana na magonjwa ambayo hayakugharimu fedha nyingi kutibiwa.

Kage na wasomi wenzake walifaulu katika kuikomboa jamii dhidi ya ufisadi. Waliliafikia hili kupitia kwa kufichua unyakuzi wa ardhi ya Halmashauri ya jiji iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya umma. Baada ya juhudi zao, ardhi hii ilirudishwa na wanyakuzi hao kuchukuliwa hatua za kisheria. Vilevile, Kage, Nafula na Makena walifaulu katika ukombozi dhidi ya uozo wa jamii. Kage alifanya hivi kupitia kwa kufichua jinsi mamake alivyouliwa kikatili kupitia kwa njama iliyopangwa na babake kwa jina Mbogo. Mbogo alihukumiwa kifungo cha maisha kwa uovu huu na kuwa funzo kwa wengine waliokuwa na mienendo kama yake.

Kwa upande mwingine, Nafula alichangia katika ukombozi dhidi ya uozo wa jamii kupitia kwa kumfichulia Daktari Makau ukweli kuhusu uasherati wa Agutu aliyekuwa mpenzi wake na ambaye alikuwa tayari ameambukizwa virusi vya UKIMWI. Kwa bahati nzuri, Daktari Makau alithibitisha kuwa hakuwa amepatwa na janga hili baada ya kupimwa na hivyo basi wakaachana.

Hata hivyo, nadharia tete hii haikuafikiwa kikamilifu kwa kuwa ukombozi wa kisiasa baada ya uhuru (ukombozi dhidi ya ukoloni mamboleo) haukupatikana katika jamii ya *Wimbo Mpya* kwa kuwa wapiganiaji uhuru waliokuwa wamesalia msituni baada ya uhuru ili kuendelea na vita hadi pale ambapo serikali mpya ingetimiza ahadi zao baada ya uhuru ili uhuru kamili na wa kweli kupatikana walitawanyika na kurudi makwao. Hii ilikuwa baada ya ujumbe kutoka kijijini kwenda kumrudisha nyumbani Marete aliyekuwa kiongozi wa kikosi cha vita kwa ajili ya ugonjwa wa mke wake. Kuanzia siku hiyo, vita vya ukombozi baada ya uhuru vilifikia kikomo.

Nadharia tete ya tatu ilikuwa “Mikakati ya kujikomboa wanayoitumia wanajamii wa *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* itafanikisha ukombozi.” Utafiti huu ulibainisha kuwa kufanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa wanajamii husika katika juhudi zao za ukombozi kulitokana na mikakati chanya ya kujikomboa waliyoibuni wanajamii wenyewe. Mikakati iliyohusisha uundaji wa majeshi ya vita ya kupigania uhuru na uundaji wa vyama vya kisiasa kama vile UWATA ilileta ufanisi mkubwa. Chama hiki cha upinzani kilileta mabadiliko makubwa baada ya uchaguzi

mdogo wa eneo bunge la Rware ambapo kilipata ushindi mkubwa dhidi ya chama tawala. Vilevile, shirika la JEMA liliundwa kwa ajili ya utunzaji wa mazingira yaliyokuwa yameharibiwa. Akina mama nao waliunda kikundi chao kilichoanzisha miradi ya kiuchumi iliyowaletea fedha nyingi. Aidha, mikakati ya ufichuzi wa ardhi ya umma iliyokuwa imenyakuliwa na Kipanga ilifanikisha ukombozi dhidi ya ufisadi.

Ujenzi wa shule ya msingi ya Gaito ulikuwa mojawapo ya mikakati ya ukombozi wa kielimu kwa kuwa huduma za elimu zililetwa karibu na wanakijiji na watoto wakaacha kutembea masafa marefu wakienda shule. Vilevile, mikakati ya kupeleka matibabu ya bure vijijini ilifanikisha ukombozi dhidi ya umaskini na magonjwa. Kufichuliwa kwa maovu yaliyokuwa yakiendelea katika jamii kulifanikisha ukombozi dhidi ya uozo wa jamii.

### 4.3 Hitimisho

Madhumuni ya utafiti wetu yalikuwa kutathmini changamoto zinazozikumba jamii za *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*, kuchunguza aina tofauti za ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti* na kisha kuonyesha mikakati ya kujikomboa wanayoitumia wanajamii wa *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Kutokana na muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu, ni dhahiri kuwa changamoto zilizozikumba jamii hizi husika ndizo zilizopelekea katika harakati za kujikomboa. Aidha, utafiti huu umeonyesha kuwa jamii hizi zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika juhudi zao za ukombozi kwa kuwa mikakati ya kujikomboa waliyoitumia wanajamii hawa ilikuwa chanya na ya kutegemewa.

### 4.4 Mapendekezo kuhusu tafiti za baadaye

Ili utafiti wowote uweze kuwa wa manufaa kwa jamii, ni sharti mtafiti aweze kutambua pengo ambalo linahitaji kuzibwa na watafiti wa baadaye. Kuhusiana na haya, tumetoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa baadaye:

i. Tafiti nyingine zifanywe kwa kutumia nadharia nyingine za kutafiti vipengele mbalimbali kama vile mtindo.
ii. Watafiti wengine waweze kutafiti kuhusu nafasi ya vijana katika ukombozi wa jamii katika riwaya hizi kwa kuwa utafiti wetu umejikita katika nafasi ya jamii nzima katika ukombozi.

## MAREJELEO


Chacha, W.C. (2013). Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama ee*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa**.**

Cheche, B. (2009). Utu wa Mtu Unadhihirika Katika Utunzaji wa Mazingira katika Jarida la *Umaskini na Mazingira*. Toleo la 7: 6-10. Tanzania: Periplus Ltd.

Eagleton, T. (2011). *Why Marx was Right*. New Haven: Yale University Press.

FAO, (2011). *State of the World's Forests.* Food and Agricultural Organization of the United Nations: Rome.

Karanja, P.N. (1990). Tamthilia za Kiukombozi, Taswira ya Mwafrika Katika Vita vya Ukombozi dhidi ya Ukoloni. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kiango, S. D. (1993). *Nadharia Mbalimbali Katika Uhakiki*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Kilabuko na Madete, (2010). Uchafuzi wa Hewa Unavyoathiri Maendeleo Katika Jamii Katika *Jarida la Umaskini na Mazingira.* Toleo la 7: 10-12.Tanzania: Periplus Ltd.

Kiongera, K. J. (2012). Mchango wa Vijana Kuleta Mabadiliko Chanya katika Tamthilia Teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kipyegon, E. K. (2013). Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke Katika *Natala* na *Kifo Kisimani.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Lunacharsky, A. (1973). *Literature and Art (2nd* Edition). Moscow: Progress Publishers.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Marx, K. (1959). *Marx and Engels on Literature*. New York: International General.

Mazrui, A. (1984). Uhakiki wa *Dunia Mti Mkavu*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi na Nadharia*. Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishing.

___________ (2004*). Wimbo Mpya*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

___________ (2010). *Msururu wa Usaliti*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mugambi, E. K. (1983). Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.

Mugambi, P. M. (1982). Uhakiki wa Maudhui Katika Tamthilia za Kiswahili za Kikenya Zilizochapishwa. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Murungi, G.K. (2013). Mtindo Unavyoendeleza Maudhui Katika *Natala.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Muthuki, J.M. (2006). Rethinking Ecofenism: Wangari Maathai and the Green Belt Movement in Kenya. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kwazulu – Natal (Howard College Campus) katika www, academia.edu /6253747/ The Green Belt Movement Ecofeminist of Wangari Maathai.

Nelleman, et.al (2009). *The Environmental Food Crisis – The Environment's Role in Adverting Future Food Crisis.* A UNEP rapid response assessment. Norway: Birkeland Trykkeri.

Njogu, K. (1987). Maudhui ya mapinduzi katika Riwaya za Visiwani Zanzibar. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Nyerere, J. K. (1967). *Elimu ya Kujitegemea*. Dar es Salaam: Mpiga Chapa wa Serikali.

Osango, D. S. (2015). Ukombozi wa Kisiasa na Kiuchumi Katika *Mkamandume*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Sabula, M. A. (2014). Nafasi ya Wanawake Katika Uhifadhi wa Mazingira Katika Riwaya ya *Nakuruto.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Sarara, M. M. (1997). Maudhui Katika Tamthilia za S.A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es salaam: Press and Publicity Centre.

Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

UNICEF (2010). *Child Friendly Schools Manual*: UNICEF- Kenya.

UNICEF (2012). *Progress for Children: A report card on adolescents, no. 10*: New York. University Press.

Wa Mberia, K. (1997). Natala. Nairobi: Marimba Publications.

___________ (2001). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications.

Wafula, R.M. na Kimani, N. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, S. (2006). *KCSE Revision History and Government.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi; Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

___________ (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia. Nairobi*: Focus Publishers Ltd.

___________ (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

___________ (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Williams, R. (1977). *Marxism and Literature*. London: Oxford University Press.

World Bank (1992). *World Development Report: Development and the environment*. Oxford